# ULINGANISHI WA MATUMIZI YA TASFIDA ZA MUKTADHA WA NYUMBANI KATIKA LUGHA YA KIKAMBA NA KISWAHILI

**NA**

**NGUTI MARY**

**C50/65661/2011**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**IDARA YA KISWAHILI**

**OKTOBA 2013**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo kingine chochote kile, kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili

Sahihi ………………………….. Tarehe ………………………………

**NGUTI MARY**

**Mtahiniwa (C50/65661/2011)**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi …………………………… Tarehe ………………………………..

**DKT. IRIBE MWANGI**

**(Msimamizi**)

Sahihi …………………………….. Tarehe…………………………………

**DKT. AYUB MUKHWANA**

**(Msimamizi)**

## TABARUKU

Kazi hii naitabarukia marehemu babangu John Nguti Mwaniki, mamangu mpendwa Esther Kalunda na mwandani wangu Josai Mwanganda.

## SHUKRANI

Ebenezah! Ninasema. Umbali huo Mungu ndiye aliyeniongoza, kuniangazia, kunifunulia na kunipa siha njema kuendelea na kufika mahali nimefika. Bila uwezo wa Mungu singeweza. Sifa, shukrani, utukufu na heshima ni zake.

Katika pilkapilka zangu za kuishughulikia kazi hii, wengi wamenifaa kwa sako na bako kwa njia tofautitofauti. Kwa kweli ni mdeni kwa wengi kwa msaada wao wa hali na mali ambao kwazo nimefaidika kuikamilisha kazi hii pasipo kuzama kwenye tope la sahau na la kunata.

Hii kazi ingeniwia nzito nisiweze kuinua kufikia upeo huu. Shukrani tele! Nawavulia kofia na kuwapigia saluti wasimamizi wangu Dkt. Iribe Mwangi na Dkt. Ayub Mukhwana kwa uongozi wao tangu mwanzo hadi tamati ya tasnifu hii. Uvumilivu wao, uelekezi na uongozi ulinifungua macho kiusomi kwa njia ya kipekee.

Shukrani tele kwa wahadhiri wengine walioniandaa kufikia kuikabili kazi hii ya kitaaluma namna hii. Wahadhiri, Prof. John Habwe, Prof. Mwenda Mbatia, Prof. Kineene wa Mutiso, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Zaja Omboga, Dkt E. Mbuthia, Dkt. Swaleh Amiri na Mwalimu B. Mungania.

Hongera mume wangu Josai Mwanganda kwa kunilipia karo, kunitia moyo mambo yaliponiwia mazito, kunishauri na kunipa msaada wa hali na mali. Watoto wetu Purity na mume wake Peter, Esther, Hussein na Rusley kwa kunivumilia waliponihitaji kwa mambo mengi. Changamoto kwao ni kuwasihi wasome hadi upeo wa maisha.

Shukrani maalumu kwa marehemu Ruth Njiru(Gatondo) mwalimu aliyenifungua macho kwa kunielekeza jinsi ya kujiunga na chuo kikuu.

Isitoshe, shukrani sufufu kwa watumishi wa Mungu walioniombea, Rev. Alex, Pastor Kivuitu na wahudumu wa kanisa la KCCC. Waombezi wote kwa jumla, pamoja na

WOPRANET, Debora (pst.wambui, Evaline, Irine na Lydia). Marafiki zangu Joyce mulinga, Phyllis, Beatrice, Caro na Jane Gitonga asanteni sana kwa kusimama katika mwanya na kuhakikisha nimeikamilisha kazi hii. Mama mkwe Mary Mkabili Mungu akubariki kwa kuniombea na kunipa motisha. Ndugu zangu na watoto wao nawashukuru pia kwa kunielewa na kunitia moyo kuendelea.

Shukrani maalum ziwaendee familia ya Bw. na Bi.George Arita na watoto wao. Mlinifaa kuliko ndugu. Mbarikiwe sana.

Shukrani tele ziwaendee wazamili wenzangu ambao kwangu walinifaa kupita kiasi, mlikuwa msaada kwangu, urafiki, upendo, uchangamfu na undugu wenu uliniwezesha kufaulu na kuibuka salama.

Dada Ruth katutu, rafiki yangu wa karibu, maombi na motisha uliyonipa ilinifaa, Juliet, Lilly, Moraa, Meroline, Grace, Ann, Rose, Njeri, Anjela, Chepng'tich, Florence, Ndugu Ndumbu, Makange, Owala, Ogutu, Onyonka, Mutoka, Murithi, Keter, wahamasishaji wetu Chacha na Muniu (mlitushughulikia kwa moyo mkunjufu). Mola awakirimie neema tele. Jane na Wambui kwa kupiga chapa kazi hii kwa makini, nawapa heko! Asanteni nyote.

# IKISIRI

Tasnifu hii imeshughulika na kulinganisha matumizi ya tasfida katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili. Ingawa tasnifu hii imetolewa kwa mahitaji ya shahada ya Kiswahili, data iliyochanganuliwa ni kutoka lugha ya Kikamba na ya Kiswahili. Uchanguzi huu tuliufikia kwa kutambua umuhimu unaostahili kupewa lugha zetu nyingine za Kiafrika katika muktadha wa nyumbani na miktadha mingine mbalimbali.

Kwa sababu ya juhudi zinazofanywa na kila jamii kuikuza na kustawisha maadili katika maisha ya binadamu wote (Stockwell, 2008). Ndiposa tukawa na jukumu la kuchunguza matumizi ya tasfida za nyumbani. Somo la tasnifu hii ni ulinganishi wa matumizi ya tasfida katika lugha ya Kikamba na Kiswahili katika muktadha wa nyumbani.

Tumechunguza matumizi ya tasfida kwa lugha ya Kikamba na kulinganisha na matumizi katika lugha ya Kiswahili. Hatukulinganisha matumizi ya tasfida katika lugha hizi mbili kwa kutaka kulingamisha tu bali, kwa kufanya hivyo tumetoa mwanga zaidi kuonyesha kuwa, tasfida ni chombo muhimu na maalum cha mawasiliano katika jamii yoyote. Tumeonyesha kwamba jamii mbili zinazotofautiana kwa mengi huweza kuwa na mawazo sawa kuhusu jamii na mazingira yao kwa jumla.

Madhumuni makuu katika tasnifu hii yalikuwa kulinganisha matumizi ya tasfida katika lugha hizi mbili, Kikamba na Kiswahili ili kudhibitisha kuwa, kunao uhusiano mkubwa katika matumizi ya tasfida. Tumechambua jinsi matumizi ya tasfida hufanikisha mawasiliano katika lugha ya Kikamba na Kiswahili. Tulikuwa na shabaha pia ya kuchunguza jinsi hali za jamii kama umri, Kazi, jinsias na hadhi huathini matumizi ya tasfida.

Data ilikusanywa kupitia mahojiano na hojaji zilijazwa na watafitiwa wateule. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa na kubainishwa kwa msingi wa nadharia ya Upole iliyoasisiwa na Penelope Brown na Levinson (1978).

# YALIYOMO

Ungamo ........................................................................................................ ii

Tabaruku ........................................................................................................ iii

Shukrani ........................................................................................................ iv

Ikisiri ........................................................................................................ vi

Vifupisho ........................................................................................................ xii

**SURA YA KWANZA**

**ULINGANISHI WA MATUMIZI YA TASFIDA ZA NYUMBANI KATIKA LUGHA YA KIKAMBA NA KISWAHILI**

1.0 Utangulizi ........................................................................................................ 1

1.1 Tatizo la utafiti ........................................................................................................ 5

1.2 Madhumuni ya Utafiti ........................................................................................................ 6

1.3 Nadharia tete ........................................................................................................ 6

1.4 Sababu za kuchagua mada ........................................................................................................ 6

1.5 Upeo na mipaka ........................................................................................................ 7

1.6 Msingi wa kinadharia ........................................................................................................ 8

1.7 Yalioandikiwa kuhusu Mada ........................................................................................................ 12

1.8 Mbinu za Utafiti ........................................................................................................ 14

1.9 Hitimisho ........................................................................................................ 19

**SURA YA PILI**

**DHANA YA TASFIDA NA UAINISHAJI WAKE KIMAKUNDI**

2.0 Utangulizi ........................................................................................................ 20

2.1 Ufafanuzi wa Dhana ya Tasfida ........................................................................................................ 20

2.2 Uainishaji wa Tasfida ........................................................................................................ 23

2.2.1 Tasfida Chanya na Tasfida Hasi ..... 23
2.2.2 Tasfida Ng'amuzi na Tasfida Ng'amuzibwete ..... 25
2.2.3 Tasfida Misimu na Tasfida Endelezi ..... 27
2.2.4 Tasfida za Desturi na Tasfida Zisizo za Desturi ..... 29
2.2.5 Tasfida za Kikazi/Taaluma ..... 30
2.2.6 Tasfida za Kujamiana ..... 31
2.2.7 Tasfida za Magonjwa ..... 32
2.2.8 Tasfida za kifo ..... 32
2.2.9 Tasfida za Anatomia ..... 33
2.2.10 Tasfida za Takamwili ..... 34
2.11 Hitimisho ..... 35

**SURA YA TATU**

**MATUMIZI NA UPANUZI WA TASFIDA ZA NYUMBANI KATIKA LUGHA YA KIKAMBA NA KISWAHILI**

3.0 Utangulizi ..... 36
3.1 Kitendo cha Usemi ..... 36
3.1.1 Matumizi ya Tasfida ..... 38
3.1.2 Kanuni za Matumizi ya Tasfida ..... 39
3.2 Matumizi ya Tasfida kutokana na Mazingira ..... 40
3.2.1 Matumizi ya Tasfida za Sehemu za Siri za Wanaume na Wanawake ..... 43
3.2.2 Matumizi ya Tasfida za Hedhi kwa Wanawake ..... 46
3.2.3 Matumizi ya Tasfida katika Sherehe za Harusi na Nyimbo ..... 48
3.2.4 Matumizi ya Tasfida za Desturi na zisizo za Desturi ..... 50
3.2.5 Matumizi ya Tasfida za Kikazi/Taaluma ..... 53
3.2.6 Matumizi ya Tasfida za Majina ya Wanajamii ..... 55

3.2.7 Matumizi ya aina mbalimbali za Tasfida zilizotokana na Data ya Kutangamana ....................56

3.3 Hitimisho ....................58

**SURA YA NNE**

**MASIALA YA KIJAMII KATIKA MATUMIZI YA TASFIDA**

4.0 Utangulizi ....................60

4.1 Athari za Umri, Jinsia Kazi na Hadhi katika Matumizi ya Tasfida ....................60

4.1.1 Umri....................61

4.1.2 Jinsia ....................62

4.1.3 Kazi ....................63

4.1.4 Hadhi ....................63

4.2 Jinsi Tasfida hufanikisha mawasiliano....................65

4.2.1 Maoni ya watafitiwa kuhusu matumizi ya tasfida katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili. ....................66

4.2.2 Maoni ya watafitiwa kuhusu nyakati tofauti tofauti ambazo tasfida hutumika..69

4.2.3 Maoni ya watafitiwa kuhusu matumizi ya tasfida kama chombo cha kufanikisha na kuathiri mawasiliano ....................72

4.3 Tasfida za Majina ya jamii kwa lugha ya Kikamba na Kiswahili. ....................73

4.4 Tasfida za Ujauzito....................74

4.5 Tasfida za kujamiana....................75

4.6 Tasfida za Magonjwa ....................76

4.7 Tasfida za kifo....................77

4.8 Tasfida za Anatomia na Sehemu za siri za binadamu. ....................78

4.9 Tasfida za Takamwili ....................79

4.10 Uchanganuzi wa Data....................80

4.10.1 Uchanganuzi wa Data kutokana na Wanaume(Kikamba) ............................80
4.10.2 Uchanganuzi wa Data kutoka kwa wanaume(Kiswahili) .............................81
4.10.3 Data ya matumizi ya Tasfida za nyumbani katika lugha ya Kikamba. ..........84
4.10.4 Data ya matumizi ya Tasfida za nyumbani katika lugha ya Kiswahili. .........86
4.10.5 Data ya matumizi ya tasfida za nyumbani katika lugha ya Kikamba. ...........88
4.10.6 Data ya matumizi ya Tasfida za kinyumbani katika lugha ya Kiswahili…...89
4.11 Muhtasari wa matokeo ya Data......................................................................93
4.12 Hitimisho .........................................................................................................94

**SURA YA TANO**

**MUHTASARI WA MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

5.0 Utangulizi .........................................................................................................95
5.1 Muhtasari wa Matokeo ........................................................................................95
5.2 Changamoto za Utafiti.........................................................................................97
5.3 Mapendekezo ........................................................................................................98
MAREJELEO ...........................................................................................................100
VIAMBATANISHO………………………………………………………………102
Kiambatanisho A: Mahojiano, Sampuli ya data kutoka watafitiwa wanne

**VIFUPISHO**

| | | |
|---|---|---|
| KZ | - | Kiasi cha juu zaidi |
| KJ | - | Kiasi cha Juu |
| KK | - | Kiasi cha kadri |
| KC | - | Kiasi cha chini |
| UC | - | Upole chanya |
| UH | - | Upole hasi |
| UF | - | Upole fiche |
| K | - | Kuheshimu |
| KS | - | Kuficha siri |
| H | - | Hazitumiki |
| KM | - | Kuepuka miiko |
| BM | - | Bila mpango |
| FZ | - | Hufanikisha zaidi |
| AZ | - | Huathiri zaidi |
| Alama | - | √ (mkakati uliotumika) |

# SURA YA KWANZA

# ULINGANISHI WA MATUMIZI YA TASFIDA ZA NYUMBANI KATIKA LUGHA YA KIKAMBA NA KISWAHILI

## 1.0 Utangulizi

Kikamba ni lugha inayozungumzwa na watu waitwao Akamba na kwa umoja *Mukamba*. Neno hili limeswahilishwa kuwa Wakamba. Wakamba wanaishi katika eneo lililokuwa mkoa wa mashariki wa nchi ya Kenya (Mathoko 2004). Mahali wanapoishi panaitwa Ukambani (Ndeti 1972). Kulingana na mapokezi ya baadhi ya sehemu za Ukambani, neno *Mukamba* linatokana na neno *amba* lenya maana ya kusema. Mwanzo wa Wakamba kuitana hivi ni wakati walipokuwa wakigawanyika kutoka sehemu walipokaa mwanzo huko milima ya Ulu (Kyulu) huko Machakos ambapo walihamia kutoka Kiima Kyeu (Mlima Mweupe) yaani Kilimanjaro.

Walipotoka sehemu zile walianza kubishana wao wenyewe waende upande upi, ndipo ukazuka usemi kuwa *"Inywi mwiamba ata? Ko mwi andu ma kuamba kuamba?" kumaanisha Sasa nyinyi mnasema nini? Kwani mmekuwa watu wa kusema sema tu?* (King'ei 1982)

Wakamba wamo katika kundi la Wabantu liitwalo Wabantu wa mashariki ambalo kulingana na wanahistoria walipitia kaskazini kutoka Shungwaya. Hata hivyo Wakamba wenyewe hupinga madai hayo wakidai walitoka sehemu ya Kilimanjaro kupitia sehemu ya Utaita na kupitia Kusini mashariki sehemu za Mbooni na Kilungu (King'ei 1982). Wakamba ni wazungumzaji wa lugha ya bantu na wameainishwa katika kikundi kimoja

na Wagikuyu, Wameru, Watharaka, Waembu na Wambeere wajulikanao kama *Central Bantu cluster* (Guthirie 1948).

Jamii ya Wakamba hupatikana katika Kaunti za Machakos, Kitui na Makueni. Wengine wamo katika eneo la Mwea Kaunti ya Embu, Shimba hills Kaunti ya Kwale na pia sehemu za Taita Taveta na Mombasa (Kitavi 1992, (Maundu 1980) na (Mathooko 2004).

Mto Athi huigawa ardhi inayomilikiwa na Wakamba katika sehemu mbili. Upande wa Magharibi na Mashariki mwa Mto Athi, kuna Kaunti za Makueni na Machakos. Kusini Mashariki kunayo Kaunti ya Kitui. Wakamba wamepakana na Wagikuyu, Wambeere, Waembu na Watharaka upande wa Magharibi. Sensa ya idadi ya watu nchini Kenya inaonyesha Wakamba walikuwa karibu milioni tatu katika mwaka wa (1999). Upangaji wa kabila za Kenya kulingana na idadi unaonyesha kabila linaloongoza kwa wingi ni Wagikuyu (5.5M), Wakalenjin (5M) Wajaluo (3.5M) halafu Wakamba (3M) ambao wako nambari ya tano. Hili ni kulingana na serikali ya Kenya Kitengo cha *Kenya Bureau of statistics* (1999).

Lugha ya Kikamba ina lahaja mbalimbali. Mutiga (2002) ameainisha lahaja tano za Kikamba; mbili za Kitui, moja ya Machakos, moja ya Makueni na moja ya Mwingi. Maundu (1980) alitambua lahaja nne za Kikamba ambazo ni:

a) Lahaja ya Mwingi
b) Lahaja ya Kitui
c) Lahaja ya Kilungu
d) Lahaja ya Machakos.

Katika utafiti wake wa baadaye, Maundu (1986) alitambua lahaja tano zinazozungumzwa katika Kaunti ya Kitui na mbili zinazozungumzwa Kaunti ya Machakos na Makueni. Hivi leo, Wakamba wanaishi kama jamii moja ya watu wazungumzao lugha ya Kikamba yenye lahaja nyingi. Hata hivyo hapana pingamizi baina ya lahaja hizi zote yenye kutatiza kusikilizana kwao (King'ei 1982). Wakamba ni wafugaji wa mifugo, wawindaji, wafugaji wa nyuki, wakulima wa mahindi, mtama na maharagwe (Kapiyo 1996). Sehemu wanazoishi ni kavu kwa hivyo mara kwa mara wanakuwa na uhaba wa mvua na kukumbwa na baa la njaa.

Kwa upande mwingine, asili ya neno "Swahili" kama Whiteley (1969:2) anavyodokeza ni Kiarabu. Swahili ina maana ya pwani au miji ya pwani. Neno hili kama maneno mengine baada ya kuingizwa katika lugha za Kibantu limenyambuliwa kwa njia mbalimbali na kwa maana mbalimbali. Neno Mswahili linasimamia watu wa pwani na Kiswahili ikawa lugha ya wenyeji wa pwani. Hata hivyo kumekuwa na mgogoro kuhusu maana ya Mswahili na Waswahili.

Stigand (1913:116) asema kuwa, Mswahili ni mtu mwenye asili ya Kiarabu au Mlowezi wa Kiarabu kutoka sehemu ya Uajemi.

Edward Steere (1870) aliandika na kusema "Sharti ikumbukwe kuwa Mswahili ni mtu mwenye mchanganyiko wa damu ya Mwafrika na Mwarabu." Kutokana na maoni ya wataalamu hawa wawili, na wanayoiendeleza ni kuwa asili ya Waswahili inatokana na Waarabu ambao waliingiliana na Waafrika kindoa. Whiteley (1969:7 – 8) alisema, "Si vigumu kuona maoni ambayo yametolewa kuwa Kiswahili ni mchanganyiko wa lugha ya Kiarabu ………si lugha halisi……….haina sarufi wala fasihi".

Maoni ya aina hii yanajitokeza katika maandishi ya Susan Fuller (1967) ambaye aliandika makala yake katika gazeti la Times Educational Supplement na kusema; Ushirikiano wa muda mrefu kati ya Waarabu na Wabantu ulizaa lugha ya Kiswahili..

Chiraghdin na Munyapala (1977) na Mwita (1992) wanasema jina la Kiswahili lilitumika kwa mara ya kwanza na msafiri mmoja kwa jina Ibn Batuta ambaye alitembea Pwani ya Afrika mashariki katika karne ya kumi na nne. Neno hili lilitumiwa kumaanisha eneo la pwani ya Afrika. Lilitumiwa kwa maana mseto kwa kumaanisha lugha, watu na mambo ya pwani. Kwa hivyo, Kiswahili kinyume na nadharia mbalimbali zilizoendelezwa kuhusu chanzo chake ni lugha ya watu maalumu walio wenyeji wa sehemu maalumu yaani Pwani ya Afrika Mashariki.

Lugha hii ilitumiwa kueleza mawazo na mazingira ya kiupwa. Baadhi ya wasomi hudai kwamba Ibn Batuta alimaanisha kwamba Uswahilini ni Kusini mwa Mombasa. Mutahi (1986) ameshikilia kuwa Kiswahili ni lugha moja kati ya lugha za Sabaki yaani lugha zinazozunguka Mto wa Sabaki na bonde lake. Ametumia ushahidi wa Kiisimu na utafiti wa wataalamu wengine kama; Heinebusch, Nurse na Phillipson (1973) kudhibitisha msimamo wake wa asili ya Kiswahili kuwa Mto wa Sabaki katika nchi ya Kenya.

Mto huu una majina mengi lakini jina lililoshamiri sana ni Mto Athi. Sehemu inayozungumziwa kuwa chanzo cha Kiswahili ni sehemu ya Ozi Karibu na Amu ambayo kutoka kale ilijulikana kama Uswahilini. Kwa hivyo Kiswahili ni lugha ambayo chiimbuko lake ni sehemu za pwani ya Afrika Mashariki hata ingawa wataalamu katika taaluma hii hawajaafikiana kuhusu sehemu yenyewe hasa. Lugha hii kabla ya kuwasili kwa wageni ilikuwa ikitumiwa na wenyeji wa mwambao katika shughuli zao za

mawasiliano ya kila siku kama lugha nyingine yoyote, waliitumia katika mawasiliano yao ya kibiashara kama Ibn Batuta anavyotodokezea. Leo hii Kiswahili ni lugha ambayo imeenea sana na inazungumzwa na watu wengi. Inakisiwa kwamba idadi ya wazungumzaji wa lugha hii ni zaidi ya milioni hamsini na ni lugha ya saba ulimwenguni.

## 1.1 Tatizo la utafiti

Mada ya utafiti huu inahusu ulinganishi wa matumizi ya tasfida za nyumbani katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili. Kulingana na Stockwell (2008), kunayo maneno ya mwiko yanayotumika na kushtua wazungumzaji na wasikilizaji. Hivyo basi matumizi ya maneno kama haya huwafanya wazungumzaji kuyafunika kwa kutumia maneno ya tasfida na ya kukopwa kwani yana upole kiasi. Jambo hili ni muhimu hasa katika juhudi ambazo kila jamii hutia ili kustawisha na kukuza misingi ya maadili katika maisha ya kila binadamu.

Ni kwa sababu hii ya kutaka kukuza maadili basi tutakuwa na jukumu la kuchunguza matumizi ya tasfida za nyumbani na iwapo tasfida hizi zina uhusiano wowote katika lugha hizi mbili. Katika matumizi ya tasfida pia maswala ya jinsi tasfida hufanikisha mawasiliano yatachunguzwa kwani tasfida huwa zimeundwa kutokana na utamaduni ambao huwasilishwa na lugha ya jamii husika, (Franz 1978). Utafiti huu utakuwa na jukumu la kuchunguza iwapo hali za watu kama umri, kazi jinsia na hadhi zao wanapotumia tasfida huweza kuyaathiri matumizi ya lugha au la.

## 1.2 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu umetathmini ulinganishi wa matumizi ya tasfida zitumiwazo katika muktadha wa nyumbani katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili. Kutokana na shabaha hii madhumuni mahususi ya utafiti huu yatakuwa:

1. Kulinganisha uhusiano wa matumizi ya tasfida zitumiwazo katika muktadha wa nyumbani katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili.
2. Kuchunguza kama tasfida zitumiwazo katika muktadha wa nyumbani zaweza kufanikisha mawasilino.
3. Kuchunguza jinsi hali za kijamii kama umri, kazi, jinsia na hadhi za watu huweza kuathiri matumizi ya tasfida katika muktadha wa nyumbani.

## 1.3 Nadharia tete

Katika utafiti huu tumeongozwa na nadharia tete zifuatazo:

1. Kunao uhusiano mkubwa katika matumizi ya tasfida zitumiwazo katika muktadha wa nyumbani katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili.
2. Matumizi ya tasfida katika muktadha wa nyumbani hufanikisha mawasiliano.
3. Umri, jinsia, kazi na hadhi ni masiala ambayo huathiri matumizi ya tasfida katika muktadha wa nyumbani.

## 1.4 Sababu za kuchagua mada

Tumeichagua mada hii kwa sababu lugha hutumika kuashiria mfumo jamii wa jamii husika; kwa hivyo kuna uhusiano baina ya lugha na jamii ambamo lugha hiyo hutumika,

(Harry 1954). (Franz (1978) anasesma lugha inayotumiwa na watu wote katika jamii ndiyo hasa hubeba utamaduni wa watu hao.

Kulingana na Hymes (2000) utamaduni ni jumla ya matatizo, kaida, malengo na maadili yanayotambulisha asasi, shirika, au kundi fulani la watu. Mamoridou (2000) naye anasema kwamba lugha huchukuliwa kama mojawapo ya kipimo katika kufanikisha mawasiliano na katika hali hii mchakato wa habari ambao ndio mawasiliano hufanyika.

Kulingana na misingi ya kazi hizi za kina Harry (1954), Franz (1978), Hymes (2000) na Marmoridou (2000), ni kweli kabisa tasfida kama kipengee cha lugha katika jamii huundwa na utamaduni wa jamii husika. Matumizi ya tasfida katika lugha basi hutegemea jinsi utamaduni ulivyomuumba binadamu wa kike na wa kiume. Matumizi ya tasfida katika muktadha wa nyumbani katika jamii hizi mbili za Kikamba na Kiswahili yatategemea jinsi utamaduni umewaumba binadamu wa jamii hizo. Ni kwa sababu hii basi tasfida katika muktadha wa nyumbani katika lugha ya Kikamba na Kiswahili zitatafitiwa ili kuchunguza kama kunao uhusiano wowote katika matumzi yake. Tutatathmini pia ufaafu wa tasfida hizo hasa miongoni mwa watumizi wa lugha hizi mbili. Tumetambua kwamba kazi hii ya kulinganisha tasfida za lugha ya Kikamba na ya Kiswahili haijashughulikiwa na kwa hivyo kunao mwanya ambao tutaziba kiusomi.

**1.5 Upeo na mipaka**

Utafiti huu umetathmini uhusiano uliopo katika matumizi ya tasfida za nyumbani katika lugha ya Kikamba na Kiswahili. Katika utafiti wetu tumechambua tasfida hamsini za Kikamba na kuzilinganisha na hamsini za Kiswahili. Tumekusanya tasfida mia moja lakini kwa sababu ya muda na upeo wetu imetubidi kushughulikia chache tu.

Tumeshughulikia matumizi pekee wala hatukuzungumzia swala la uteuzi kwa sababu ya muda kama tulivyosema hapo awali.

Tasfida hizi zimekusanywa katika wadi ya Wote kaunti ya Makueni. Hii ni sehemu mojawapo ambapo wazungumzaji wa lugha ya Kikamba huishi. Tasfida za Kiswahili nazo zimekusanywa wadi ya Kibokoni kata ya Mvita sehemu mojawapo ambapo Waswahili huishi. Tumelenga aina za familia kwa jumla yaani familia dogo na familia pana. Vijana ambao wamelengwa ni wa miaka 18-35 kina mama na wanaume – miaka 30- 70.

Maelezo mengine ya tasfida huenda yakapatikana kwa nyimbo za sherehe za muktadha wa nyumbani na iwapo patakuwa na haja nyimbo hizo zitaelezwa na kuandamanishwa. Tumezichagua tasfida zetu kutokana na mambo, kazi sherehe na hali za nyumbani.

**1.6 Msingi wa kinadharia**

(Harry 1954), anasema kwamba lugha ndiyo huashiria mfumo jamii wa jamii husika na jamii ambapo lugha hio huzungumzwa, kama tulivyosema hapo awali, ili kuchunguza ulinganishi wa matumizi ya tasfida ambazo ni sehemu ya lugha na utamaduni, tutatumia nadharia ya upole na mikakati ya uso chanya na uso hasi.

Kulingana na Mayumi (2006) fasiri nyingi zimetolewa kuhusiana na nadharia hii ya upole ambazo sio dhahiri kwa kufasiri neno upole. Hata hivyo, tafiti hizi za Magharibi na za Japan hazikutofautisha upole kutoka kwa maneno mengine kama kuonyesha heshima, adabu na ukawaida ambayo hutumiwa badala ya upole

Upole kulingana na Mayumi basi huangaliwa kwa njia mbili. Kwanza njia kuu na pana ni kuangalia mitazamo tofauti na upana wa nadharia za upole. Kwa njia nyingine ndogo na bayana humaanisha mikakati ya upole kama ulivyoelezwa na Brown na Levinson (1978)

Penolope Brown na levinson Brown (1978) walisema kila binadamu anapenda kutambuliwa kwa yale anayosesma. Hivyo basi binadamu ana:- Uso chanya na Uso hasi ambazo anaweza kuzihifadhi au kuzipoteza kwa sababu ni kitu cha kihisia. Wanasema kwamba katika maisha ya kila siku watu hujaribu kuunda na kubuni habari ambazo zinahifadhi nyuso za wengine na kukamilisha mikakati mingine. Binadamu huzihifadhi nyuso kwa sababu anataka kumfanyia mwengine heshima

Waandishi hawa wanaamini kwamba upole ni mkakati kwa sababu una umuhimu sana katika tamaduni kwa jumla. Tamaduni tofauti tofauti zina viwango tofauti tofauti vinavyohitajika na pia njia tofauti tofauti za kuwa na upole. Watu wote wana sababu za kukubalika na nyuso zao kuhifadhiwa.

Upole ni jambo la muhimu hasa katika mawasiliano ya kila siku. Tunapokosa kutimiza mahitaji ya uso chanya na hasi katika mazungumzo tunafanya kosa la kuvuruga matendo na mikakati ya uso. Kuvuruga matendo ya uso ni kawaida lakini lazima mikakati fulani itumiwe ili kuepuka shida katika matokeo yake.

Kuna njia nyingi za kushughulikia matendo ya uso. Hatuishughulikii kwa njia moja bali kwategemea upole utakaotumika na kwa njia zipi na jinsi gani. Kuna mikakati mitano ambayo hutumika. Mifano ya mikakati hii ni:

1. Mikakati bayana, huu ni mkakati ambao hauna tendo la upole

2. Uso chanya
3. Uso hasi
4. Ujumbe fiche
5. Kutowasilisha kabisa

**Mfano wa Mkakati Bayana**

Mtoto anayetaka kununuliwa nguo ya Sikukuu na baba yake atamwambia, ‘ningependa uninunulie nguo ya Sikukuu.” Maneno haya hayana upole na baba anaweza kuhisi mtoto amemkosea heshima. Pengine mtoto angeandamanisha maneno yale na upole kiasi na kusema, “nitashukuru sana kama utaninulia nguo ya Sikukuu,” mama alisema wewe hununua nguo nzuri sana. Huku ni kuuliza lakini kumeandamanishwa na upole wa kumsifu baba. Itafaa zaidi kama itaandamanishwa na upole hasi. Mfano “Samahani najua huna pesa lakini naomba nikusumbue; nitashukuru sana kama utaninunulia nguo ya Siku kuu.” Maneno haya yanatimiza mahitaji ya uso hasi kwani yametumia maneno ya kuomba msamaha na kumsifu baba pia.

**Mkakati wa Ujumbe Fiche**

Mkakati wa Ujumbe Fiche hauko wazi, kwa mfano; mke anaweza kusema “Sijui nitazifanyia nini nywele zangu zimefumuka mno.” Mke akimweleza mume maneno haya anakusudia mume atapata fununu na kuelewa kwamba anahitaji fedha za kwenda kusukwa nywele.

**Mkakati wa Uso Chanya**

Uso chanya una haja ya kukubalika, kutambulika na kuheshimika. Mkakati wa uso chanya umeundwa ili kutimiza mahitaji haya. Kwa mfano, unaonyesha uhusika au kuhusika na hali ya mwingine kwa kumpongeza na kwa kutumia maneno ya heshima. Mfano, "Umevalia mavazi nadhifu, wapendeza sana." Maneno haya yanaonyesha kutambulika, kupendeka na kukubalika mno.

**Mkakati wa Uso Hasi**

Uso hasi ni ile hali ya kutamani kuwa huru pasipo kuingiliwa. Hivyo basi uso hasi hutumiwa ili kuhifadhi uso wa mwingine wakati mahitaji ya uso hasi yamevurugwa. Kwa mfano "Samahani kwa kukusumbua lakni unaweza kunieleza sufuria ya mtoto iko wapi?" Tayari mlengwa ameombwa msamaha asisumbuliwe katika hali yake asiyopenda ikivurugwa.

Kulingana na Penelope na Lenvinson (1978) mikakati ambayo hutumiwa hutegemea fomula fulani ambayo hufafanuliwa kama jumla ya kazi. Maneno ya upole ambayo mtu huamua kutumia hutegemea uhusiano wa mzungumzaji na msikilizaji na pia hutegemea mamlaka ya msikilizaji kuliko ya mzungumzaji na hatari iliyoko katika kumuudhi mwingine. Kwa mfano, ukitaka kumwomba ndugu yako kitu kisichohitaji upole na mamlaka sawa ombi lako halivurugwi kwa hivyo utatumia upole kiasi tu. Mfano mwingine, ukitaka kumwomba mkopo mzazi wako kwa sababu yuko na ngazi ya juu kukuzidi utakuwa na upole zaidi.

Nadharia hii imetumika katika kuchanganua data kwa kuangalia ni vipi tasfida hutumika na hutumia mikakati ipi. Nadharia hii pia imetumika kama mizani kuonyesha kwamba tasfida zatumiwa kuhifadhi uso chanya na uso hasi.

## 1.7 Yaliyoandikiwa kuhusu Mada

Katika matumizi ya kawaida ya lugha Fromkim na Rodman (1988:189) wanasema kwamba jamii katika hali yake ya uvumbuzi wa lugha hubuni maneno na kisha huamua nini chafaa kuzungumzwa kwa upole na nini hakifai. Wanadai kwamba maneno yote yako wazi kwa mzungumzaji ili ayatumie lakini muktadha wa jamii huamua kile husemwa, na kisemwe wapi na lini. Wanaendelea kusema uchafu na urembo wa lugha hutambulika katika sikio la msikizaji au sikio la jamii nzima kwa jumla. Tunakusudia kulinganisha lugha katika jamii mbili tofauti lugha ya Kikamba na Kiswahili kwa hivyo walichokiandika kuhusu lugha na jamii kitatufaa.

(Hymes 1964) kwa kumnukuu Nadel (1954), na pia Wardhaugh (2002) amewataja Wanupe wa Afrika Magharibi kama mojawapo wa watu wapole ulimwenguni kwa kufanya uteuzi mwafaka wa maneno yanayofaa zaidi na yasiyofaa kaika mazungumzo. Wao huamua kutumia tasfida moja kwa moja ili kutaja sehemu nyeti za mwili.

Trudgill (2002:58) anasema kwamba katika jamii nyingi mazungumzo ya jinsia tofauti, vyeo na umri hutofautiana na sio kwa hayo tu bali pia hutofautiana kulingana na muktadha wa kijamii ambapo mzungumzaji hujipata. Maelezo haya yatakuwa ya manufaa kwetu kwani tutachunguza jinsi hali za jamii lugha zikiwemo, umri, kazi, jinsia, na hadhi huathiri matumizi ya tasfida katika muktadha wa nyumbani.

Njeri (2007) alichunguza tasfida katika mazungumzo kuhusu virusi vya ukimwi na kusema kwamba kunao wakati ambapo tasfida hukwamiza mawasiliano hasa pale ambapo pana uana, umri hata kazi wazifanyazo wazungumzaji na wasikilizaji. Anasema ingawa tasfida hutumiwa kama mikakati ya kupunguza athari hasi baadhi yazo zina athari za uso bado. Utafiti huu utatufaa kwani waonyesha matumizi ya tasfida katika lugha ya Kikuyu na katika hali tofauti ya ugonjwa wa Ukimwi. Tofauti na utafiti wetu unao shughulikia ulinganishi wa matumizi ya tasfida katika lugha mbili tofauti, Kikamba na Kiswahili.

Mukaria (2011) anazungumzia aina tofauti za tasfida anapoandika kuhusu maneno ya miiko na tasfida katika lahaja ya Kiimenti. Tasnifu hi itatufaa kwa sababu imeziainisha tasfida katika makundi tofauti nazo tasfida zetu zitahusu sajili ya nyumbani kwa Kiswahili na Kikamba.

Wambua (2009) alitatifi kuhusu tofauti ya matumizi ya kilahaja na mitazamo za leksika za miiko na tafsida katika jamii ya Kikamba. Aliweza kutofautisha jinsi mitazamo tofauti inavyojitokeza katika matumizi na maana ya leksika za miiko na tasfida kwa kulinganisha lahaja za lugha ya Kikamba. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu umeshughulikia miiko na tasfida na kutumia nadharia tofauti na yetu, hata hivyo utatufaa kwa kuwa umeshughulikia tasfida za lahaja mbili za Kikamba, na Kikamba ni moja wapo ya jamii lugha tunayoitafitia

Mutiso (2005) katika makala yake ya *The Nature of Forbidden Language* amezungumzia maneno ya miiko ambayo hutumiwa katika lugha ya Kikamba hasa katika hali ya kumdunisha mwanamke. Kazi yake hii itatufaa kwani yeye tofauti nasi ameshughulikia

jinsia ya kike kwa kuilinganisha na ya kiume. Kwa kuonyesha jinsi jinsia moja imedhalilishwa, nasi tutagusia kwa kiasi jinsi matumizi ya tasfida huathiriwa na jinsia.

Mutiga (2002) katika uchunguzi wake wa Toni za Kikamba lahaja ya mwingi alizitaja pia lahaja tano ambazo huzungumzwa katika eneo la Ukambani kwa jumla na akimrejelea Maundu (1980) amezitaja lahaja hizo tano kama:

1. Lahaja ya Mashariki na Kitui
2. Lahaja ya Kitui  Kati
3. Lahaja ya Kitui Kaskazini
4. Lahaja ya Machakos (inayoitwa kimasaku)
5. Lahaja ya Kilungu ambayo huzungumzwa Makueni.

Kazi yake ingawa haijazungumzia tasfida imetaja lahaja ya Kikilungu ambayo ni Kikamba ambacho huzungumzwa Makueni wadi ya Wote ambayo ni sehemu moja ya utafiti wetu. Kwa sababu amezungumzia toni za lahaja ya Mwingi tunaweza kufaidika kwa mwongozo tu bali lahaja hii ni tofauti na ya Makueni, aidha hatuwezi kutumia tasfida pasipo toni.

### 1.8 Mbinu za Utafiti

Utafiti wetu umefanyika nyanjani. Utafiti huu umefanywa katika Wadi ya Wote Kaunti ya Makueni na Wadi ya Kibokoni kata ya Mvita Mombasa. Wadi hizi mbili zimechangia katika kulinganisha matumizi ya tasfida kwa mujibu wa nadharia ya upole iliyoasisiwa na Penelope Brown na Stephen Levinson (1978). Data iliyokusanywa ni ya matumizi ya tasfida za nyumbani katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili. Data hii imekusanywa katika Wadi ya Wote Kaunti ya Makueni na Wadi ya Kibokoni kata ya Mvita. Matumizi

haya ya tasfida za nyumbani yamehusishwa na mikakati ya nadharia ya upole iliyoasisiwa na Penelope B na Levinson S (1978). Mikakati hii ni pamoja na uso Hasi, Uso Chanya na mkakati Fiche.

**Aina za Utafiti**

Njia iliyotumiwa katika utafiti huu ilikuwa ya ufafanuzi. Njia hii inajaribu kuchunguza jinsi kitu au hali ilivyo kwa wakati fulani na kuifafanua lugha na kuripoti jinsi ilivyo. Pia hujaribu kutafuta ukweli wa aina tofauti (Kothari 2004). Mugenda na Mugenda (2003) wanasema mbinu hii ya ufafanuzi humwezesha mtafiti kushughulika na kueleza hali ya vitu au matukio wala hana uwezo juu ya viathiriwa. Mtafiti hupima vipengele au kukadiria vipengele. Mfano, ni mara ngapi kitu hutokea.

**Data na Njia za Kukusanyia Data**

Kiini cha data tuliyoikusanya ni kutaka kulinganisha matumizi ya tasfida za nyumbani tukijikita katika lugha ya Kikamba na Kiswahili.

Nicholas Walliman (2005) anasema kwamba njia hii ya ufafanuzi inahusu zaidi kutazama kama njia ya kukusanyia data. Njia ya kutazama inaweza kujitokeza katika hali kulingana na utafiti unaofanywa. Hali hizo ni kama: mahojiano ya ana kwa ana, hojaji ambazo hutayarishwa na kupewa watafitiwa ili waweze kuzijaza. Yanayosikilizwa pia huandikwa na mwisho kufafanuliwa kama data.

Data imekusanywa kwa njia ya mahojiano ya ana kwa ana ambapo mtafiti ameuliza maswali moja kwa moja bila kutumia hojaji. Haya ni mahojiano ambayo yanamfaa mtafiti kwani atabainisha ufasiri wa matumizi ya tasfida kwa watumizi lugha ya Kikamba

na ya Kiswahili. Maswali haya pia ni ya wazi na humwezesha mtafiti kupata habari nyingi zaidi kutoka kwa mtafitiwa. Njia ya kujaza hojaji imetumiwa pia kukusanyia data. Hojaji zilitayarishwa na kupewa watafitiwa ili wazijaze. Sehemu moja ya hojaji ina maswali ambayo yaonyesha viwango tofauti vya matumizi ambavyo vyatumika kama kipimo ili kutathmini maoni ya watafitiwa.

Kipimo hiki ndicho kimetumiwa;

1. Kiasi cha chini (KC)
2. Kiasi cha kadiri (KK)
3. Kiasi cha juu (KJ)
4. Kiasi cha juu zaidi (KZ)

Data pia imekusanywa kwa njia ya kutazama, kusikiliza na pia kwa njia ya kushiriki. Kulingana na Kothari (2004) data inayokusanywa kwa njia hii huhusishwa moja kwa moja na matukio katika wakati uliopo. Tumetumia hatua za kusikiliza, kuandika na kujaza hojaji katika kukusanya data.

**Vifaa vya Kukusanyia Data**

Hojaji

Kalamu na karatasi

Kutazama na kutangamana

Kwa sababu ya swala la tamaduni, pale mwanamke haruhusiwi kupata habari nyingi kutoka kwa mwanamme ambaye si mumewe, msaidizi wa kiume anayefahamu lugha, tamaduni, desturi na mila za Kiswahili alitafutwa ili kumsaidia mtafiti ambaye ni wa

kike. Mtafiti msaidizi huyu alifunzwa jinsi ya kuwahoji walengwa na mtafiti mkuu na kisha apewa jukumu la kuwatafsiria watafitiwa hojaji ili waweze kuelewa. Mtafiti msaidizi wa lugha ya Kikamba hakuhitajika kwani mtafiti ni mzaliwa wa Ukambani na anaweza kujieleza kwa lugha ya Kikamba na anazielewa mila, desturi na tamaduni za Kikamba.

**Sampuli ya Watafitiwa na idadi**

Sampuli kulingana na Mugenda na Mugenda (2003) ni sehemu ndogo ya idadi jumla ya utafiti. Naye Nicholas Walliman (2005) anasema kwamba sampuli ni kiasi cha watafitiwa ambacho huchaguliwa kutokana na idadi kubwa. Sampuli hufanywa tu pale ambapo kundi kubwa huwakilishwa na kundi dogo la kutafitiwa

Tumeichanganua data kwa kutumia sampuli ya kundi au kishada kulingana na Kothari (2004). Sampuli kundi au kishada huweka kundi kubwa kwa makundi madogo madogo ambayo huitwa vishada badala ya watu binafsi. Kundi moja huwakilisha kikundi kikubwa kwa sababu huwa na sifa ambazo kwa kiasi kikubwa zafanana.

Vikundi hivi hugawanywa kisha kikundi kimoja huchaguliwa. Tutatumia sampuli hasibu ili kupata idadi ya kutafitia.

Mwisho mtafiti hutumia sampuli ya kusudi ili kukusanya data kwa watu wa familia tofauti.

Mugenda na Mugenda (2003) wanasema kuwa idadi ya watafitiwa ni idadi jumla ya vikundi, vitu au matukio ambayo yana sifa bainifu zinazofanana. Katika utafiti wetu idadi jumla ya watafitiwa ni watu wa familia kwa jumla yaani familia ndogo na familia pana

ambao wana umri wa miaka 18-70. Hii ni kwa sababu watu wa umri huu wana uelewa zaidi wa lugha waizungumzayo. Katika kila familia iliyochaguliwa kupitia njia ya sampuli ya kusudi, tuliwahoji vijana au mtoto mmoja, mama, baba, babu na nyanya iwapo wapo. Kwa jumla tuliwahoji watafitiwa watano kwa kila familia moja teule.

Sampuli yetu ilikuwa watu wa familia ndogo na wa familia pana. Sampuli hii imetoka wadi ya Makueni ambayo ina idadi ya familia 13,432 na wazungumzaji wa Kiswahili wadi ya kibokoni ambapo kuna famila 8,106 kulingana na Sensa ya Serikali ya Kenya ya (2009). Familia hizi ziligawanya kwa kutumia sampuli kishada katika wadi kisha tukatumia sampuli ya kusudi katika kuchagua namba ya watafitiwa kwa sababu ya swala la muda.

**Njia za Kuchanganua Data**

Data zimechanganuliwa kwanza, kuthibitisha kama kunao uhusiano wowote katika matumizi ya tasfida za lugha ya Kikamba na Kiswahili kulingana na madai ya kwamba tasfida kama kipengee cha jamii huundwa na utamaduni jamii husika na matumizi yake hutegemea jinsi utamaduni ulivyomuumba binadamu wake (Harry 1954, Fran 1978, Hymes 2000 na Marmondou 2000).

Data imechanganuliwa na kubainishwa kwa msingi wa nadharia ya Upole. Data hizi zitawekwa kwa makundi mbalimbali kutegemea aina za tasfida, matumizi, athari na ufanisi wake katika mawasiliano.

Uchanganuzi huu wa data umefanywa kwa njia ya kiasilimia ambao umelinganisha matumizi ya tasfida za Kikamba na za Kiswahili, athari za hali tofauti na jinsi matumizi ya tasfida hufanikisha mawasiliano.

### 1.9 Hitimisho

Sura hii ya kwanza imeshughulikia mambo ambayo ni ya kiutangulizi tu kama vile: utangulizi, tatizo la utafiti, sababu za kuchagua mada, nadharia tete, upeo na mipaka, msingi wa kinadharia wa utafiti na njia za utafiti. Sura hii itakuwa msingi wa sura zifuatazo kwani zitaegemea katika mhimili wa sura hii.

Sura ya pili imeshughulikia ufafanuzi wa dhana ya tasfida na aina tofauti za tasfida. Uanishaji wa tasfida utakuwa msingi wa uchunguzi wetu wa kulinganisha matumizi ya tasfida za muktadha wa nyumbani katika lugha ya Kikamba na Kiswahili kwa sura ya tatu na ya nne.

## SURA YA PILI

## DHANA YA TASFIDA NA UAINISHAJI WAKE KIMAKUNDI

### 2.0 Utangulizi

Katika sura hii tumefafanua dhana ya tasfida kulingana na yaliyoandikwa kuhusu msamiati wa tasfida. Tumeeleza aina mbalimbali za tasfida kwa kuangalia uainishaji wa tasfida na kutoa mifano kutoka lugha ya Kikamba na ya Kiswahili. Maelezo haya ni ya muhimu kwani ndiyo yatakuwa msingi wa sura ya tatu ambapo tutashughulikia matumizi ya tasfida.

### 2.1 Ufafanuzi wa Dhana ya Tasfida

Dhana ya tasfida imeelezwa na Wanaisimu wengi kwa njia tofauti tofauti. Kwa mfano, Allan na Burridge (1991) wanasema kwamba neno tasfida ambalo ni tafsiri ya kutokana na *'uephemism'* hutokana na uambatanishi wa viambajengo vya kigiriki*'eu'* kumaanisha 'nzuri' na '*pheme*'ambalo humaanisha kuzungumza. Kwa hivyo neno tasfida kwa tafsiri ya '*eupheme*' humanisha kuzungumza kwa maneno mazuri au kuzungumza kwa usemi usioudhi na kumdhuru mtu.

Gatambuki (2009) akirejelea mawazo ya Bright (1985) na Allan na Burridge (1991) anaeleza kuwa tasfida ni kutumia maneno mazuri, matamu, yanayopendeza, yaliyotiwa nakshi yakavutia. Pia anasema ni kutokusema maneno moja kwa moja ili kuepuka kudhuru uso wa msikilizaji.

Harry (1954) anasema kwamba lugha huashiria mfumo jamii wa jamii husika, na kwa hivyo kuna uhusiano wa lugha na jamii ambapo lugha hiyo hutumika. Katika kila jamii

huwa kuna namna lugha hutumiwa na kuleta aibu ama hata kuwa vigumu kuyatumia maneno fulani katika lugha kwani ni mwiko. Kwa sababu hii watumizi lugha huweza kukwepa hali hiyo kwa kutumia lugha inayoonekana nzuri au yenye adabu nayo huitwa tasfida. Hivyo basi tasfida ni maneno yenye adabu.

Tunakubaliana na maelezo hayo kwa sababu utafiti wetu ulidhihirisha kwamba watumizi lugha ya Kikamba na Kiswahili huunda tasfida kutoka kwa mazingira yao ili waweze kuwasiliana kwa urahisi, kwa upole na kwa adabu. Hivyo basi tunaweza kusema tasfida ni maneno yanayoundwa na kila jamii ili kurahisisha mawasiliano, kuyafanikisha na pia kuhifadhia uso wa wanaowasiliana.

Katamba (1985) anaeleza tasfida kama neno linalotumika kufafanulia lugha, mawazo na dhana ambazo hupunguza uchukivu unaoletwa na tamaduni za jamii au kundi lolote la watu.

Kwa kweli katika mawasiliano kunaweza kuzuka hali za kutoelewana kutokana na matumizi ya lugha isiyo na adabu au hata miiko. Tunakubaliana na Katamba (1985) kwamba tasfida zinapotumiwa hupunguza kutoelewana na uchukivu unaotokana na matumizi ya miiko kwa kutojali wengine.Tasfida ni neno la upole na upole huzuia chuki na kutoelewana kwa wanajamii.

Ortony (1993) naye anasema tasfida ni kule kusema kitu kwa namna ambayo mtu huchukua tahadhari ili asiseme mambo ambayo huchukiza na kumwaibisha yeye mwenyewe au hadhira yake.

Leech (1983) anaeleza tasfida kama ile hali ya kutoa maana hasi na kutia maneno urembo na nakshi ili yaonekane kuwa mazuri. Anaelezea zaidi kwa kusema kwamba mambo haya huwa katika kila jamii kutoka zamani ili kukwepa mijadala ambayo haifurahishi wengine.

Mambo kama ngono, kifo, magonjwa na sehemu tofauti za mwili wa binadamu huwa miiko na kuifanya jamii lugha kuunda tasfida ili kuwasiliana kwa upole.

TUKI (1990) inasema tafsida au usafidi ni matumizi ya maneno ya staha badala ya yale halisi. Kwa mfano, aga dunia ni neno la staha na lenye upole linalotumika badala ya neno kufa.

Wardhaugh (2002: 238) anasema lugha ya tasfida huruhusu watumizi lugha kufunika hali katika maisha na kuziwasilisha kwa njia ifaayo, kwa upole na kwa njia kubalifu kwa hadhira. Tasfida huruhusu wanajamii kuzungumza vitu visivyofaa kwa njia ifaayo ili kuvipunguza makali. Kwa mfano tasfida hutumika katika kueleza kitendo cha kujamiana, kifo, hedhi, magonjwa na sehemu za siri za binadamu. Tasfida pia huwawezesha watumizi lugha kuvipa vitu visivyofaa vibandiko na hata majina ya kuvifanya vipendeze.

Ullman (2005) anasema kwamba kila utamaduni huwa na mambo ambayo hayazungumzwi wazi ambayo huitwa miiko. Haya ni mambo au chochote kilichokatazwa katika jamii kwa sababu za kidini au za kiutamaduni. Katika matumizi ya lugha watu huyakwepa matumizi ya miiko na kujikita kwa kutumia lugha inayoonekana kuwa nzuri katika miktadha tofauti kulingana na mazingira, na hii ndiyo huitwa tasfida.

Kutokana na utafiti wetu tumetambua kwamba tasfida huundwa na watumizi lugha wa jamii yenye utamaduni mmoja. Tasfida hizi huundwa kama njia mojawapo ya kueleza mambo au kusema jambo kwa njia ya kutumia maneno au lugha kwa upole na adabu. Ili kuficha mambo yanayoonekana mabaya au yanayoaibisha na kudunisha, tasfida hasi hutumiwa kama njia ya kupunguza makali ya maneno kwa upole na adabu ili kuhifadhi uso wa mtu mwingine.

## 2.2 Uainishaji wa Tasfida

Kuna aina nyingi za tasfida. Zifuatazo ni aina mbalimbali za tasfida;

### 2.2.1 Tasfida Chanya na Tasfida Hasi

Rawson (1981) aliainisha tasfida katika kategoria chanya na hasi, hata kama yaliyotasfidiwa yanahusiana na mwiko au la. Tasfida chanya kulingana na Rawson hutiwa chuku na huonekana muhimu sana kuliko vile zilivyo. Rawson anadai kuwa Waingereza na Wamerikani hupendelea tasfida ambazo zimetiwa chuku hasa kutasfidi kitu ambacho hakipendezi na kinadhuru.

Rawson pia anasema kuwa tasfida zinazohusu watu wanaofanya kazi ndogondogo na duni huinua hadhi ya kazi hizo ili kustiri uso wa wafanyikazi wa kazi hizo au kuzifanya kazi zenyewe zionekane nzuri. Maneno ya tasfida chanya hutiwa nakshi katika matumizi ya misamiati ya kisiasa, kijeshi na ya kibiashara.

Mfano katika lugha ya Kikamba

**<u>Tasfida Chanya</u>**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **1.** | **<u>Kikamba</u>** | **<u>Akiki</u>** | **<u>Kiswahili</u>** |
| | *(i) Kũthũania na sua* | koΘoania na sua | Kutokomea machweo na jua |
| | (ii)*Kũlea liu* | kolɛa liu | Kukataa chakula |

Tasfida hizi *kuthuania na sua* na *kulea liu* zimetiwa chuku ambapo kifo kimefananishwa na kutokomea macheo na jua na kukataa chakula. Kwa kweli mtu afapo huwa hajakataa chakula wala kutokomea na jua.

**Mfano katika Kiswahili**

**2. Kiswahili**

(i)Askari - Kwa maana ya Bawabu

(ii)Msaidizi - Kwa maana ya Yaya

Tasfida hizi zimetumiwa kwa kutia chuku ambapo Yaya ameitwa msaidizi ilhali Yaya ni mfanyikazi wa nyumbani. Bawabu naye amefananishwa na askari ambaye ana kazi nzuri na ya mshahara mkubwa kwa kutia chuku tu.

Tasfida hasi kwa upande wake hudunisha na hufanya kitu au mtu aonekane duni. Kwa ujumla tasfida hasi ni tasfida ya kujikinga na kusitiri uso, kwa kuondoa uwezo wa maneno ya miiko kwa kutumia lugha kwa kitu ambacho watu huona hakifai na hawawezi kukisema hadharani. Tasfida hasi zinaweza pia kuitwa tasfida za utamaduni au tasfida zilizobanwa, kwani ni kongwe sana. Hata ingawa tasfida hizi ni hasi bado zinahifadhi uso wa msikilizaji na pia zina upole kuliko maneno halisi ya miiko.

Katika utafiti wetu tulitofautisha tasfida hasi na chanya na kuona kwa kweli tasfida hasi zilikuwa zikitumiwa sana na watu wazima kuwaelekea watu wa umri mdogo.

**Tafsida hasi**

**3.**

| **Kikamba** | **Akiki** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| *(i)Katũmbũlũ* | katombolo | Sehemu ya tupu ya mbele ya mwanamke |
| (ii) *Mbaki* | mbake | Tumbako (sehemu ya siri ya kike kwa kuidunisha |

*Katumbulu* ni sehemu ya tupu ya mbele ya mwanamke kwa kuidunisha. *Mbaki* nayo ni sehemu ya siri ya kike au ya kiume kwa kuidunisha. Hizi ni tasfida zinazotumiwa kuonyesha upole hasi lakini kwa njia ya kuzidunisha.

Mfano katika lugha ya Kiswahili

**4. Kiswahili**

*(i) Kisima*

*(i) Kinu*

*Kisima* na *kinu* ni tasfida za sehemu za siri za mwanamke ambazo zimefananishwa na vitu ambavyo huenda chini. Hii ni katika hali ya kudunishwa.

### 2.2.2 Tasfida Ng'amuzi na Tasfida Ng'amuzibwete

Tasfida hata ikiwa hasi na chanya huweza kuainishwa kama tasfida ng'amuzi na tasfida ng'amuzibwete. Tasfida ng'amuzi ziliundwa kitambo sana hivi kwamba ni watu wachache huweza kukumbuka asili yazo. Watu huzitumia pasipo kujua kama wanazitumia na pasipo kujua kama kuna kitu wanachokiepuka na kukiwepa (Rawson 1991).

Mfano wa tasfida ng'amuzi katika lugha ya Kikamba ni,

| | Kikamba | Akiki | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 5. | *(i) Kwona mwei* | kwɔna mwɛi | Kuona mwezi kwa maana ya kuwa na hedhi |
| | *(ii) Kũtwaa ndii mwakoni* - | kotwaa ndii mwakɔni - | kupeleka nyuzi mjengoni, kwa maana ya kufa |

Tasfida hizi ni za zamani na watumizi lugha walizizoea. Tasfida hizi kwao ni kama maneno ya kawaida kwani yanaashiria hali ya kila wakati kwa kila mwezi kwa mwanamke. Kuona mwezi ni jambo la kawaida katika kila jamii, hali hii imezoeleka. Kupeleka nyuzi mjengoni nayo ni hali ya kawaida kwani mtu huenda na kurudi tu. Kama vile hali hizo katika jamii zimezoeleka ndivyo tasfida hizo huzoeleka.

Mfano katika Kiswahili

**6. Kiswahili**

(i) Kuona mwezi – Kumaanisha hedhi

(ii) Mvua – kwa maana ya hedhi

Kulingana na Gatambuki (2009), kinyume na tasfida ng'amuzi tasfida ng'amuzibwete hutumika sana na huhusisha kategoria changamano. Watu wanapowasiliana na wengine, wazungumzaji huwa na ufahamu wa tasfida ng'amuzibwete kwa hivyo huzitumia kwa uangalifu na msikilizaji huelewa maana iliyokusudiwa.

Mfano katika lugha ya Kikamba:

| 7. | **Kikamba** | **Akiki** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| | *(i) Kũtwa mata* | kotwa mata | Kutema mate, kwa maana ya kukojoa |
| | *(ii) Kwĩtethya* | kweteϴja | Kujisaidia, kwa maana ya kwenda haja ndogo au kubwa |

Mfano katika lugha ya Kiswahili:

**8. Kiswahili**

*(i) Kujisaidia* – kwa maana ya kwenda haja ndogo au kubwa

*(ii) Kwenda msalani*- kwa maana ya kwenda chooni.

### 2.2.3 Tasfida Misimu na Tasfida Endelezi

Gatambuki (2009) anasema tasfida zaweza pia kuainishwa kwa uwezo wazo wa kudumu au kutodumu ambao hujulikana kama misimu. Tasfida za aina hii ni zile ambazo hutumika kwa wakati fulani kisha husahaulika ama hudumisha kutegemea na matumizi. Tasfida misimu ni zile ambazo huibuka ama huundwa na kutumika kwa wakati fulani au shughuli fulani, na hiyo shughuli ikiisha nazo zinaisha au zinakufa.

Mfano katika lugha ya Kikamba

**Tasfida Misimu**

| 9. | **Kikamba** | **Akiki** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| | *(i)Kũsũvĩa Mũsyĩ* | kosovea Mosje | Kutunza familia |
| | *(ii)Mũtyethoka* | *motjɛθɔk*a | Mti wa shoka |

Tasfida hii *kusuvia musyi* ambayo ina maana ya kutenda kitendo cha ngono huwa inatumika wakati wa Sherehe za harusi na baada ya harusi tasfida hiyo husahaulika.

*Mutyethoka* nayo ni tasfida ambayo hutumiwa kwa wakati kwa kumwashiria msichana bikira na baadaye inatoweka.

Mfano katika lugha ya Kiswahili

**10. Kiswahili**

(i) Shoka- Kwa maana ya sehemu ya siri ya mwanamume

(ii) Kijiti- Kwa maana ya sehemu ya siri ya mwanamume

Tasfida hizi shoka na kijiti hutumika tu wakati wa sherehe za harusi na sherehe ikiisha hazitumiki tena.

**Tasfida Endelezi**

Tasfida endelezi nazo ni zile ambazo hukaa na kujimudu katika matumizi kwa muda mrefu.

| 11. | **Kikamba** | **Akiki** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| | (i) *Ndĩĩ* | ndee | Kinu (sehemu ya siri ya mwanamke) |
| | (ii) *Ng'a Mutuku* | ŋa motuko | Mjukuu wa Mutuku. |

Mifano tulioitoa hapa kama *Ng'a Mutuku* ni tasfida hupewa mkaza mwana na bavyaa au mavyaa wake na kuanzia siku hiyo huendelea kuitwa kwa jina hilo.

Mfano katika lugha ya Kiswahili.

**12. Kiswahili**

(i) Kinu- Kwa maana ya sehemu siri ya mwanamke

(ii) Kitwangio- Kwa maana ya sehemu ya siri ya mwanamume

Tasfida hizi ziliundwa wakati wa sherehe za harusi na kuendelea kutumika hadi sasa.

### 2.2.4 Tasfida za Desturi na Tasfida Zisizo za Desturi

Levinson (2002) anadai kuwa kipragmatiki, tasfida zaweza kuainishwa kama tasfida za desturi na tasfida zisizo za desturi. Tasfida za desturi ni zile ambazo umaanisho wake tayari umepata mizizi. Mtindo wa kuandika na maana ya kipragimantiki tayari imepata mizizi kwa matumizi na huwa dhana ya maana ndiyo imeachwa. Kwa kuwa umaanisho wake umepata mizizi, sitiari ya tasfida hizi yaweza kutambulika maana inayokusudiwa kipragimantiki kwa urahisi.

Kwa mfano tasfida za desturi

Kikamba

| **13.** | **Kikamba** | **Akiki** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| | *(i) Ena aeni* | ɛna aɛni | Ana wageni kumaanisha ana hedhi |
| | *(ii) Nunatethekie* | nonateθɛkiɛ | Alisaidika kwa maana ya alizaa |

Mifano katika Kiswahili

**14. Kiswahili**

(i) Alijifungua - kwa maana ya alizaa

(ii) Ameleta kipya - kwa maana ya amezaa

Tasfida hizi zinapotumiwa huwa zinatambulika tu kwani kila watumizi lugha huzielewa pasipo matatizo.

Tasfida zisizo za desturi nazo huwa hazijakomaa na umaanisho wake huwa unategemea muktadha, kwa hivyo bila kuwa na msingi kamili wa ufahamu na umakini wa muktadha unaweza kupata ugumu kuelewa au kupata umaanisho wa tasfida hizi.

Kwa mfano katika Kikamba:

| **15.** | **Kikamba** | **Akiki** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| | *(i)Nũnathũmũie* | nonaθomoiɛ | Alikufa ama alizaa ama amelala |
| | *(ii) Kũkoma* | kok ɔma | Kulala, inaweza kuwa kufa au kupumzika katika usingizi. |

Mfano katika lugha ya Kiswahili

**16. Kiswahili**

(i) Amepumzika –Kwa maana amekufa

(ii) Ametuaga – Kwa maana ya kufa

Tasfida *amepumzika* inatumiwa kwa maana nyingi. Kwa mfano, amepumzika kutoka safari, kutoka kazi aliyoifanya, kufa au hata kuzaa. Nayo tasfida *ametuaga* inatumiwa kumaanisha, kufa na kuonyesha kwaheri mtu akienda safari. Itamlazimu mtu kuuelewa muktadha wa matumizi ndiposa ang'amue maana.

### 2.2.5 Tasfida za Kikazi/Taaluma

Katika nchi nyingi kazi za akili huonewa fahari, nazo kazi za sulubu huonekana kama kazi duni au za watu wa tabaka la chini. Tofauti hii inapanuliwa zaidi na tofauti ya mishahara wanayopewa watu hawa. Kazi za kiakili huvutia kwa kuwa zina mishahara minono. Kazi za sulubu nazo huwa na mishahara duni. Kazi hizi duni na wanazozifanya huvutia matumizi ya tasfida ili kuficha uso au kuonyesha upole wa wafanyikazi na kazi wanazozifanya.

Mfano kwa Kikamba:

| **17.** | **Kikamba** | **Akiki** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| | *(i) Mwĩĩtu wakwa* | mwe:tu wakwa | Binti yangu kwa maana ya Yaya |
| | *(ii)* Nd*akĩtalĩ* | ndaketale | Daktari kwa maana ya Mganga |

Mfano katika Kiswahili

**18.** **Kiswahili**

(i) Daktari-Kwa maana ya Mganga

(ii) Mkunga- Kwa maana ya anayezalisha

### 2.2.6 Tasfida za Kujamiana

Swala la kujamiana ni mada ambayo ni mwiko hasa mbele ya watu, na huepukwa sana kama mada ya mjadala. Lugha ya kujamiana huibua mchezo wa maneno na lugha ya sitiari. Katika tamaduni nyingi, miiko mikali imetumika dhidi ya ngono nje ya ndoa (Allan na Burridge 1991). Hii ni njia mojawapo ya kuonya watu dhidi ya uzinifu hasa kwa wanawake. Ni kwa sababu hii basi tasfida hutumika ili kuhifadhi uso wa msikilizaji.

Mfano katika Kikamba:

| **19.** | **Kikamba** | **Akiki** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| | *(i) Kũvitya* | kovɛtja | Kutenda kosa kumaanisha mtu ametenda uzinifu |
| | *(ii) Kũkomania* | kokɔmania | kulalana, kwa maana ya kutenda kitendo cha ngono |

Mfano katika lugha ya Kiswahili;

**20. Kiswahili**

(i) Kulala - kwa maana ya kutenda kitendo cha ngono

(ii) Kukuna nazi - kwa maana ya kutenda tendo la ngono.

### 2.2.7 Tasfida za magonjwa

Watu hawapendi kuongea kuhusu magonjwa waziwazi, wengi wanaporejelea magonjwa hutumia tasfida, kwa sababu ya woga wa kifo au kwa sababu magonjwa husababisha kifo.

Kwa sababu hii watu hutumia tasfida kuepuka kudhurika au kuwadhuru wengine. Maneno kama haya hutumiwa,

Mfano katika lugha ya Kikamba

**21.**

| Kikamba | Akiki | Kiswahili |
|---|---|---|
| *(i) ĩkua* | ekua | mafua kumaanisha ugonjwa wa kisonono (unaofichwa hausemwi hadharani). |
| *(ii) Kavithe* | kaviθε | kaswende, yenye kufichwa |

Mfano katika lugha ya Kiswaliill:

**22. Kiswahili**

(i) Kuendesha - kwa maana ya kuhara

(ii) Kutokwa na maji- kwa maana ya anajikojolea.

### 2.2.8 Tasfida za kifo

Katika jamii nyingi kifo huogopewa na watu huepuka kukitaja moja kwa moja; wanapoongea kuhusu kifo wanatumia tasfida. Allan na Burridge (1991) wanasema kuwa

kifo ni janga kubwa na maneno ya kuashiria kifo ni mwiko. Kila wakati watu wanapozungumza kuhusu kifo hutumia maneno mazuri ili kupunguza woga na ukali. Gatambuki (2009) aeleza kuwa kifo ni mwiko ambao umevutia tasfida nyingi sana kuliko miiko mingine.

Mifano katika kikamba;

| **23.** | **Kikamba** | **Akiki** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| | *(i) Mũtũtiwa* | mototiwa | Aliyetuacha kwa maana ya aliyekufa |
| | (ii) Kwĩtw*a* | kwetwa | Kuitwa yaani kufa |

Mfano kwa lugha ya Kiswahili

**24. Kiswahili**

(i) Kutuaga - kumaanisha kufa

(ii) Kulala - kwa maana ya kufa

**2.2.9 Tasfida za Anatomia**

Kulingana na Mwito (2011) sio kila sehemu ya mwili wa binadanu huwa ni mwiko katika lugha. Lugha inayohusishwa na viungo vya mwili ambavyo huhusika katika ngono huweza kuangaliwa kwa maudhiko au kwa aibu na kwa hivyo huibua tasfida za viungo hivyo.

Mfano kwa lugha ya Kikamba:

| **25.** | **Kikamba** | **Akiki** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| | (i) Kwimba kithoi | kwimba keΘɔi | Kufura kifua kumaanisha matiti yameota ama amekomaa |
| | (ii) Mĩio | meĩo | Mizigo kumaanisha sehemu ya siri ya kike |

Mfano katika lugha ya Kiswahili

**26.** **Kiswahili**

(i) Kisu- kumaanisha sehemu ya siri ya mwanamme

(ii) Kitumbua- kumaanisha sehemu ya siri ya mwanamke

### 2.2.10 Tasfida za Takamwili

Mwili wa binadamu hutoa taka ambayo kwa kawaida huwa makuruhu kwa watu, na kwa sababu hii huwa ni chanzo cha aibu kwa mtu anayezungumza kuhusu takamwili moja kwa moja. Kwa sababu hii takamwili zote tatu: mkojo, kinyesi na hedhi huibua tasfida nyingi sana, kulingana na uelewa na ufahamu wazo. (Allan na Burridge 1991).

Kwa mfano katika lugha ya Kikamba:

| **27.** | **Kikamba** | **Akiki** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| | *(i) Makonyoo* | mak ɔ ɔ: | Mkojo |
| | *(ii) Matũkũ make* | matuko makɛ | siku zake kumaanisha hedhi kwa mwanamke |

Mfano katika Kiswahili:

**28. Kiswahili**

*(i) Choo* - kwa maana ya mavi

*(ii) Mvua* -kwa amaana ya hedhi kwa mwanamke

## 2.11 HITIMISHO

Kwa kuhitimisha, sura ya pili imefafanua dhana ya tasfida na kuziainisha tasfida kulingana na sifa zake na kuzitolea mifano katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili. Tumeziainisha tasfida kwa makundi yafuatayo, tasfida chanya na hasi, tasfida ng'amuzi na ng'amuzimbwete, tasfida misimu na endelezi, tasfida za desturi na zisizo za Desturi, tasfida za kikazi au taaluma,tasfida za kujamiana,tasfida za magonjwa, tasfida za kifo, tasfida za anatomia na za takamwili.

Katika sura ya tatu tutashughulikia jinsi tasfida hutumika katika muktadha wa nyumbani katika maisha ya kila siku ya binadamu na upanuzi wake.

## SURA YA TATU

## MATUMIZI NA UPANUZI WA TASFIDA ZA NYUMBANI KATIKA LUGHA YA KIKAMBA NA KISWAHILI

### 3.0 Utangulizi

Katika sura ya pili tumekwisha ifafanua dhana ya tasfida, tumeonyesha asili yake na kuainisha tasfida katika makundi mbalimbali. Tumefanya hivyo kwa kutoa mifano mbalimbali katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili.

Katika sura hii tutakuwa na lengo la kuchunguza jinsi tasfida hutumika katika muktadha wa nyumbani katika maisha ya kila siku ya binadamu na upanuzi wake. Tutafanya hivi kwa kulinganisha matumizi ya tasfida za nyumbani katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili. Tutaongozwa na nadharia ya Upole ya Penelope Brown na Levinson (1978) ambayo hutumiwa ili kutimiza shabaha tofauti tofauti kama vile, kueleza, kusisitiza, kusimulia, kuomba na kuagiza.

### 3.1 Kitendo cha Usemi

Kwa kutimiza shabaha hizi za kueleza, kusisitiza, kusimulia, kuomba na zingine ambazo hujitokeza katika lugha yoyote ile, usemi hutumiwa. Kama anavyosema (Grice 1967), nia ya msemaji yeyote anapotumia tasfida ni kuwasiliana kwa njia yenye upole. Usemi wowote ule una umuhimu ambao hutegemea nia ya msemaji. Nadharia hii ya Upole ambayo ina mikakati tofauti tofauti imetumika kufafanua matumizi ya tasfida za nyumbani katika lugha ya Kikamba na Kiswahili.

Lengo la kutumia tasfida ni kuhakikisha kwamba,vitendo vya kuzungumza vinavyonuiwa havimhathiri msikilizaji au hadhira kwa jumla. Jukumu hili haliwezi kutimizika pasipo kutumia mikakakati tofauti tofauti ya nadharia ya Upole. Kabla ya kuzungumzia matumizi ya tafsida tutagusia kwa ufupi kuhusu jinsi lugha inavyotumiwa hasa lugha ya mazungumzo.

Kitendo cha kuzungumza ni namna ya tabia tatanizi na hufuata kanuni maalumu za matumizi ya lugha. Mtu anapotoa kanuni fulani ya usemi huwa ametenda kitendo fulani. Kuna aina tatu za utendaji ambazo hutimizwa katika kutumia lugha. Kwanza, mtu akizungumza hutoa kauli inayokubalika kisarufi kulingana na lugha husika. Pili, kuna kanuni ya utumizi ambayo huonyesha madhumuni ya msemaji katika usemi wake. Kwa mfano, kuonya, kuahidi na kuuliza. Tatu ni kanuni na taadhira Kanuni, hii inahusu nia ama alichokusudia msemaji (Mary Prah 1974). Hata ingawa hatutaingilia mambo haya,ni muhimu ifahamike kwamba yanafaa katika matumizi ya kipengee chochote cha lugha kikiwemo kipengee cha tasfida.

Nia anayokuwa nayo mtumizi wa tasfida ni kuwasilisha ujumbe wake kwa lugha ya upole na kuepuka kutumia maneno ya mwiko yanayovuruga nadhania ya Upole.

Tutaongozwa na nadhania ya Upole ya Brown na Levinson (1978), kwani inazungumzia lugha katika matumizi yake. Mtu atendapo lugha huwa ametenda kitendo cha tabia tatanizi. Kitendo hiki huwa kimeambatana na kanuni maalumu za lugha yenyewe na matumizi. Kutoa kauli fulani ni kutenda kitendo fulani cha lugha. Kitendo cha lugha hudhihirika kisarufi kwa lugha inayotumika, hutenda katika hali ya matumizi na kwa sababu ya madhumuni fulani.

Madhumuni ya mzungumzaji yanadhihirika kwa msikilizaji kwa kutumia upole au kutoutumia. Tumeshughulikia lugha ya Kikamba na Kiswahili katika matumizi ya tasfida. Tumetumia nadharia hii kufafanua mikakati inayotumika. Mikakati kama Uso Hasi, Uso Chanya na Ujumbe Fiche.

### 3.1.1 Matumizi ya Tasfida

Ili tasfida itumike kama tasfida, ni lazima ikubalike na jamii yenye kuitumia. Kama tulivyosema awali kwamba tasfida huundwa na utamaduni wa jamii husika. Katika matumizi ni lazima pia pawe na neno au usemi mmoja wenye kueleweka unaomaanisha tasfida ndiposa pawe na ufanisi katika mawasiliano. Kwa mfano katika lugha ya Kikamba;

| **29.** | **Kikamba** | | **Tafsiri** |
|---|---|---|---|
| | *1.(a)Ndeto sya kuiia* | - | maneno ya kuficha |
| | *(b) Ndeto sya ndaia* | - | maneno ya heshima |

*Ndeto sya kuiia na ndeto sya ndaia* ni usemi ulio na maana sawa na neno tasfida kwa lugha ya Kiswahili.

Katika lugha ya Kiswahili tasfida ni maneno ya heshima au yenye upole. Kama tulivyotaja hapo awali kila jamii inatia juhudi katika kuboresha na kuyaendeleza maadili. Hivyo basi itawalazimisha wanajamii kutumia tasfida kama chombo cha kufanikisha mawasiliano. Katika matumizi haya basi itabidi mtumizi lugha kushughulikia nadharia ya Upole ambayo ndiyo kiambajengo katika matumizi ya tasfida ambayo hukusudia kuhifadhi uso.

Utaratibu tulioufuata katika kuchambua matumizi ya tasfida ni, kutoa tasfida kwa lugha ya Kikamba kisha kutoa tafsiri yake sabilia pasipo kugeuza maana yake. Tumeegemea

makundi ya aina za tasfida mbalimbali tuliyoyaainisha katika sura ya pili. Kisha tumelinganisha matumizi hayo na tasfida za Kiswahili.

Ili kufikia uamuzi wa maana zaidi kuhusu matumizi ya tafsida katika lugha ya Jamii fulani, ni bora zaidi kusikiliza matumizi yake kwa sadfa bila kuuliza wasemaji kukufahamisha wenyewe. Sababu ya kufanya hivi ni kwamba mtafiti anapouliza watu kumfahamisha kuhusu muktadha huenda jawabu la mtafitiwa mara nyingi likawa si dhahiri au sahihi. kwa sababu mtafitiwa anaweza kutaka kuonyesha ujuzi alio nao.

Vilevile ili kupata data ya kufaa katika utafiti mtafiti amewahoji watafitiwa wengi ili wampe matumizi ya tasfida moja ili mwishowe alinganishe jawabu zao. Jambo hili limesaidia kupata mwangaza zaidi kuhusu matumizi ya kila tasfida. Hata hivyo, tuliweza kutangamana na watafitiwa na kusikia tasfida fulani zikitumika. Ingawa uhakika wetu kuhusu maana na matumizi ya tasfida yoyote lazima utokane na ushahidi tunaopata kutoka kwa wasemaji wa zile tasfida. Mtafiti angekuwa na muda wa kutosha basi, angetumia njia ya kuwasikiliza wazungumzaji wa Kikamba na Kiswahili, kisha aifafanue data yake. Kwa kufanya hivi matokeo yake yangekuwa bora zaidi na yenye manufaa makuu.

### 3.1.2 Kanuni za Matumizi ya Tasfida

Katika kuchunguza matumizi ya tasfida za nyumbani ambazo zimetokana na utafiti wetu, inafaa itambulike kwamba mifano ya tasfida tunayotoa hapa ni ya ufafanuzi wala haitoshelezi yote yanayohitajika kuelezwa kuhusu matumizi haya. Katambuki (2009) akimrejelea Zizheng (2005) anasema kila aina ya tasfida hutumiwa kulingana na kanuni zifuatazo.

1. Kanuni ya urefu
2. Kanuni ya uzuri/starehe
3. Kanuni ya uhusiano na utangamano
4. Kanuni ya kusitiri uso

Kanuni hizi zote ni za maana lakini kwetu tumejikita kwa kanuni ya nne ya kusitiri uso/kujikinga. Dhana hii ya kuficha uso au kujikinga huendelezwa na wazo kuwa kwa kutumia tasfida mtu huweza kujenga uso chanya katika mawasiliano na huweza kujikinga na kuinua hadhi yake katika fikira za anaozungumza nao (Grice 1975). Kanuni hii inaoana na nadharia ya Upole tuliyoitumia katika tasnifu hii.

Tumetaja kwa kifupi pia kama katika matumizi ya tasfida kuna upanuaji wa maana yoyote. Ingawa kazi yetu haishughulikii maana, itakuwa vigumu kueleza matumizi pasipo kurejelea maana.

Katika utafiti wetu tulipata kuelewa kwamba maneno ya lugha yaliundwa na jamii husika ili yaweze kutumika katika kuwasiliana. Jamii ileile baadaye iligundua kwamba baadhi ya maneno yana ukali mwingi katika matumizi, kisha wakaunda tasfida ambazo zamaanisha jambo lilelile lakini kwa upole zaidi.

### 3.2 Matumizi ya Tasfida kutokana na Mazingira

Tasfida ambazo hutumika katika lugha ya Kikamba na Kiswahili huwa zimetokana na shughuli za kila siku kulingana na muktadha au kundi la wazungumzaji. Hata ingawa kuna vianzo vingi, utafiti wetu ulitambua kwamba wazungumzaji wa lugha ya Kikamba na ya Kiswahili hupata tasfida zao kutokana na vikundi vya kisosholojia na miktadha ya mazungumzo. Vile vile wao hukopa tasfida zingine kutoka kwa lugha za kigeni.

Chochote katika mazingira chaweza kutasfidiwa. Wazungumzaji wa lugha ya Kikamba huweza kubadilisha maneno ya kawaida na dhana kuwa tasfida. Kwa mfano;

**30. Kikamba**

*(i)Muthokoi*

Tafsiri- Mseto wa chakula cha mahindi yaliyotwangwa na maharagwe

*(ii) Muthi*

Tafsir*i* – Mchi

*(iii)Ndii*

Tafsiri – Kinu

*(iv)Itaa*

Tafsiri-Aina ya meza ya kitamaduni iliotengenezwa kwa kutumia miti ili kuanikia vyombo.

*Muthokoi* ni Mahindi ambayo hutiwa kwenye Kinu na kwa kutumia Mchi hutwangwa na kutolewa ngozi ya juu. *Muthi* kwa maana ya mchi umefafanuliwa kama sehemu ya siri ya mwanamme inayofanya kitendo cha kutwanga ambalo ni tendo lile la ngono. *Muthi* ni mti ulio mpana pande ya mbele ya kutwangia na nyembamba upande wa nyuma. Inatumiwa kama tasfida kwa sababu muundo wake una sura ya sehemu ya siri ya mwanamme. *Ndii* nacho ni kifaa ambacho sehemu ya mti hukatwa na kutobolewa shimo ambalo lafananishwa na sehemu ya siri ya mwanamke. Vilevile *Itaa* ni kifaa kinachotumiwa kuanikia vyombo ili viweze kukauka. Kifaa hiki nacho kinatumiwa kama tasfida ya sehemu ya siri ya mwanamke.

Mfano katika matumizi, *Muthi* mdogo ulitumiwa kuwekwa katika kikapu iwapo mume aliyeoa msichana hakuweza kutenda tendo la ngono na kupelekewa mamake na mama wa

yule binti aliyemuoa. *Muthi* ulipoonekana tu uliashiria sehemu ya siri ya mwanamme haifanyi kazi. Kifaa kidogo chenye muundo wa *ndii* ambayo haijatobolewa nacho kilipowekwa kwa kikapu na kupelekewa mama wa bibi harusi kiliashiria kwamba msichana huyo alikuwa bikira. Vilevile matumizi yake katika kunena yangeeleweka.

Itaa ni kifaa ambacho hupatikana katika mazingira ya nyumbani na kilitumiwa kuanikia vyombo. Mke fulani akitaka kuwaeleza wanawake wenzake kwa nini alichelewa kuamka anasema, *"Munduume akomie kitaani" kwa* maana kwamba mume wake alilala juu yake kuashiria tendo la ngono.

**31. Mfano katika Kiswahili**

*(i)Pilau*

*(ii)Kinu*

*(iii)Kitwangio*

*(iv)Shoka*

Waswahili hupenda sana kula chakula kiitwacho *Pilau*. *Pilau* ni wali uliopikwa kwa mchangayiko wa mchele, nyama, kitunguu saumu, kitunguu maji na viungo kadha wa kadha. Viungo hivi hupondwa kwa vifaa viwili ambavyo ni kinu kidogo na mchi au kitwangio. *Kinu* ni kifaa kilicho na shimo ambalo huwekwa viungo ambavyo hupondwa au kutwangwa kwa *mchi* mdogo ulio na muundo wa sehemu ya mwanamme ya siri. Vifaa hivi vilevile ni tasfida katika jamii ya Waswahili ambapo Kinu kidogo chafananishwa na sehemu ya siri ya kike kwa sababu ya lile shimo, mchi au kitwangio hufananishwa na sehemu ya siri ya mwanamme.

Mfano katika matumizi; ‘*Sherehe za jana usiku zilikuwa shwari,tulitwanga viungo kinu na mchi vikawaka moto’*. Maneno hayo yanaashiria kitendo cha ngono ambacho pia kimepewa tasfida nyingine ya sherehe.

*Shoka* ni kifaa cha kukata katika mazingira ya nyumbani ambacho chalinganishwa na sehemu ya siri ya mwanamme kama inavyodhihirika kwa wimbo wa harusi ya Waswahili ufuatao.

*Kataa….kata,kata*2*

*Kata husiogope..,kata*2*

*Kata mti ni wako… kata*

*Shoka tia makali…tia*

*Kataa…kata.kata*2*

### 3.2.1 Matumizi ya Tasfida za Sehemu za Siri za Wanaume na Wanawake

Kwa mfano tasfida za kikamba zinazoashiria sehemu ya siri ya wanaume ni;

**34. Kikamba**

(i*) Muti*

Tafsiri-Mti

(ii*) Itumo*

Tafsiri-Mkuki

*(iii)Iangi*

Tafsiri-Mshale

*Muti* ambayo ni mti, *Itumo* maana yake ni mkuki na *Iangi* ambayo ni mshale ni tasfida ambazo zimetumiwa kama kifaa cha kudugia ambacho chaweza kutoboa shimo. Mti, mkuki na mshale pia ni vifaa vya vita tena hatari na kwa hivyo basi vimetumiwa kama

tasfida kupanua maana. Vifaa hivi pia huonyesha kazi zinazoweza kuifanya na hivyo kulinganishwa na sehemu ya siri ya mwanamume ambayo huweza kudunga na kutoboa sehemu ya siri ya mwanamke. Tukilinganisha matumizi haya ya tasfida za sehemu za siri za wanaume katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili, tulitambua kwamba,

**35.** **Kiswahili**

*(i)Mtaimbo*

*(ii)Wembe*

*(iii)Msumeno*

*Mtaimbo*,*wembe* na *msumeno* vyote ni vifaa na kazi yake ni kuchimba na kukata na kwamba vimepewa upanuzi wa kimaana hapa kwani sehemu ya siri ya mwanamme imelinganishwa na vifaa vyenye makali ya kukatia na kuchimba. Kile kinachokatwa hapa ni sehemu ya siri ya mwanamke. Tasfida hizi zimetumika katika tamaduni na lugha mbili tofauti na matumizi yote ni sawasawa kabisa. Kwa kutaja vifaa hivi ambavyo viko katika mazingira ya Watumizi lugha huhifadhi nyuso za wengine kwani asili ya sehemu hizo huwa ni mwiko.

Tasfida tulizotolea mifano pia kwa kule kupanua maana katika matumizi huziweka katika kundi la tasfida chanya ambazo zatilia chuku na kuonekana muhimu kuliko zilivyo. Kwa kweli kazi ya sehemu ya siri sio kukata kama msumeno wembe au kutoboa kama kijiti lakini zimetumika hapa kuashiria vile kama chuku tu.

Kwa upande mwingine tulitambua kwamba tasfida zinazotumiwa kutajia sehemu za siri za Wanawake ingawa zilipanuliwa kimaana, matumizi yake yalionyesha hali ya kudunishwa au kudhalilishwa. Sehemu hizi hazitendi chochote bali hutendewa hivyo basi upole unadhihirika hapa ni Upole hasi.Mfano;

**36. Kikamba**

*(i)Ndii*

Tafsiri-kinu

*(ii)Muio*

Tafsiri-mzigo

*(iii)Mbaki*

Tafsiri-tumbako

*Ndii* ambayo ni Kinu ni kifaa cha kuingia chini, Mti hutolewa na kuchimbuliwa ngozi na shimo kutengenezwa. Shimo huwa ndilo hutiwa mchi ndani ili kutwangia mahindi. *Muio* kwa maana ya mzigo nao humilikiwa hivyo basi sehemu hii inadunishwa kwa kuwa ni mzigo wa binadamu. *Mbaki* ni tumbaku na tumbaku ni kitu cha mtu. Mbaki pia hutumiwa kuashiria sehemu ya siri kwa kuidunisha. Sehemu hizi hata ingawa zaashiria sehemu za siri kwa kuzidunisha pia zimepanuliwa kwani sehemu ya siri inalinganishwa na tumbaku ambayo huombwa, mtu huwa ana haki kupeana ama hasiipeane. *Ndii* nacho ni kifaa tena kizito kama ulivyo mzigo pia.

Mfano katika matumizi;

Mama alimwambia msichana mdogo, '*Umya mbaki vaa we*' kwa maana ya ondoa tumbaku hapa wewe, kuashiria sehemu ya siri ya mwanamke kwa kuidunisha.

*Muio* hutumiwa kama ifuatavyo;"*Nenge muio"* kwa maana ya, nipe mzigo, yaani tufanye kitendo cha ngono.

**37. Mifano ya tasfida katika lugha ya Kiswahili.**

*(i)Kisima*

*(ii)Kitabu*

*(iii)Kinu/kitwangio*

Mfano katika matumizi;

Mwanamme mmoja aliambiwa, *'Hakikisha unakunywa maji kwenye kisima chako'*.kwa maana ya, hahakikishe anatenda kitendo cha kujamiiana na mke wake pekee. Kitabu, kinu na kisima hutumiwa kutenda tendo fulani na kuifanya duni na vyote humilikiwa na binadamu.

Kwa kulinganisha sehemu hizi za siri za kike za lugha ya Kikamba na ya Kiswahili tulitambua,

Tasfida hizi kwa kweli zimepanuliwa kimaana kwa kuwa ni vifaa lakini hudunishwa katika matumizi yake. Hizi tasfida ziko katika kundi la tasfida hasi ambazo ni za kudunisha lakini bado zinahifadhi uso wa msikilizaji.

### 3.2.2 Matumizi ya Tasfida za Hedhi kwa Wanawake

Kunazo tasfida nyingine ambazo zimekuwepo tangu zamani na watumizi lugha huzitumia tu pasipo kuelewa kwamba wanazitumia. Zinatumika kama maneno ya kawaida.

Mfano;

**38.** **Kikamba**

(i)*Kuona mwei*

Tafsiri-kuona mwezi yaani kuwa na hedhi

*(ii)Kwikwata mutwe*

Tafsiri-kujishika kichwa – kwa maana ya hedhi

*(iii)Ena aeni*

Tafsiri-ana wageni -kwa maana ya hedhi

Matumizi ya tasfida hizi katika jamii lugha zote mbili yalidhihirisha kwamba mahali mwanamke hupokea hedhi mwezi ukiwa, ndipo kwa mwezi unaofuata atapokea hedhi tena. Hedhi pia hutokea kila mwezi kwa mwanamke wa kawaida.

Hivyo basi matumizi haya yamelinganishwa na nyakati ambazo Mwanamke huipokea hedhi. Kwamba atakapouona mwezi wa kawaida basi ataiona hedhi nayo.

Matumizi mengine ni kwamba mwezi hutoa mwangaza na mwangaza huonyesha na kudhihirisha ushwari. Mtu anaweza kutembea kwa kumlikiwa na mwangaza wa bala-mwezi. Mwanamke naye akiwa katika hedhi inatoa mwangaza kwamba yeye ni shwari ni mwanamke mwenye uwezo wa kupata mimba hata ingawa kwa wakati huo hana mimba.

Tasfida zingine zinazohusishwa na hedhi kwa kikamba ni *aeni* kumaanisha kuwa ana wageni. Wageni sio wa kila wakati wageni huja na kuondoka kisha kurudi tena baada ya muda mrefu. Matumizi ya tasfida hii *aeni* ingawa ina maana zaidi ya moja ikitumiwa kwa wakamba itaeleweka kama tasfida ya upole.

Mtu asemapo *'Mama huyo hajaweza kumtembelea mume wake kwa sababu ana wageni.* Usemi huu utakuwa wenye upole zaidi kuliko kusema ana hedhi, hivyo kutahifadhi uso wa huyo Mama.

Mfano katika lugha ya Kiswahili;

**39.** **Kiswahili**

*(i)Mvua*

*(ii)Mwezi*

*(iii)hedhi*

Katika Kiswahili hatukupata tasfida kama ya wageni lakini tulipata tasfida ya mvua, Mvua katika hali ya kawaida hunyesha kwa nyakati tofautitofauti. Hivyo basi, huwa kuna kipindi cha mvua na cha ukame katika maisha ya binadamu. Vilevile katika hali za kawaida za Wanawake huwa kuna ukame na unyevunyevu. Wakati wa unyevunyevu ndio wakati wa hedhi kwa Mwanamke. Matumizi ya mwezi yalikuwa sawa na matumizi ya Kikamba nayo hedhi kwa Waswahili pia ni tasfida

### 3.2.3 Matumizi ya Tasfida katika Sherehe za Harusi na Nyimbo

Kunazo tasfida ambazo hutumiwa katika sherehe mbalimbali za nyumbani ambazo zinawahusu binadamu. Sherehe kama harusi na sherehe za utumbuizo kama *wathi-wathi* ni sherehe za nyimbo za tamaduni za Wakamba ambazo ziliimbwa na vijana wa kiume na kike wakati wa jioni huku baadhi ya wazee wakiwatazama na kuwachunga ili kudumisha maadili.

Mfano wa tasfida zilizotumiwa,

**40.** **Kikamba**

*(i)Kusuvia musyi*

Tafsiri-kutunza familia

*(ii)Mutyethoka*

Tafsiri-mti unaowekwa shoka ukiwa haujatobolewa

*(iii)Nguumo*

Tafsiri-kandokando ya mto

Tasfida hizi tulisisikia kwa sherehe za harusi na pia kwa *wathi*. Mtu alipoambiwa, '*Mulwa suvia musyi* kwa maana, *Mulwa* chunga familia, ilikuwa tasfida kumaanisha

chunga sehemu ya siri ya mwanamke ambayo ililinganishwa na familia. *Mutyethoka* nao ulilinganishwa na mwanamke bikira ilhali *nguumo* ni sehemu ya siri ya mwanamke.

Upanuzi wa kimaana unadhihirika kwa kulinganisha sehemu ndogo tu ya siri na familia, mti husiotobolewa kulinganishwa na bikira na kando kando ya mto ambayo ni sehemu kubwa kwa kulinganishwa na sehemu ya siri ya mwanamke.

Mfano wa tasfida zitumiwazo na Waswahili katika sherehe za harusi na nyimbo.

**41.** **Kiswahili**

*(i)Msumeno*

*(ii)kijiti*

*(iii)Wembe*

*Wembe* ni sehemu ya siri ya mwanamme kama inavyodhihirishwa na wimbo ufuatao wa harusi.

*(a) Wimbo*

*Waja huo wembe waja*

*Mamae mwari naajitinge*

*Waja huo wembe waja……………*

Katika wimbo huu wembe umetumiwa kama sehemu ya siri ya mwanamme kijiti na msumeno pia zimetumiwa kuashiria sehemu za wanaume za siri. Tazama mifano ya nyimbo zifuatazo.

*(b) Wimbo*

*Kumea mvi si utu uzima*

*Bora mashine kuwa nzima*

*Kwenda na gogo si utu uzima*

*Bora kijiti kiwe kizima*

*(c)Wimbo*

*Sinitilie mapengo msumeno wangu*

*Kama haukereketi nitakwenda zangu*

*Sinitilie mapengo msumeno wangu*

**3.2.4 Matumizi ya Tasfida za Desturi na zisizo za Desturi**

Matumizi mengine ya tasfida za nyumbani tayari yamepata mzizi. Tasfida kama hizi zinapotumiwa hueleweka mara moja kwa sababu ni dhana tu imesalia maana imekomaa na kukolea mizizini. Tuliweza kutambua tasfida kama hizi kwa lugha ya Kikamba na hata Kiswahili.

Mifano ya tasfida za Kikamba ni kama ifuatavyo

**42. Kikamba**

(i) *Nunatethekie*

Tafsiri-alisaidika kwa maana ya alizaa

*(ii) Nutwetee mueni*

Tafsiri –ametuletea mgeni kwa maana ya amezaa

*(iii)kutambaika*

Tafsiri-kupata mtoto ambaye hajakomaa na akiwa amekufa

Tasfida ya kwanza *Nunatethekei* inatumiwa kulinganisha tendo la kuzaa kuwa la kufa kupona. Mama mja mzito akizaa kwa salama basi wanasema amesaidika.

Katika mfano wa pili, *Nutwetee Mueni*, ametuletea mgeni imelinganishwa na Mtoto kuwa kama mgeni katika kijiji hicho kwani haelewi mila na desturi isipokuwa afundishwe, sawasawa na mgeni ugenini. Itambidi mgeni kuonyeshwa na kufunzwa mambo tofauti

ugenini. *Kutambaika* nayo ni tasfida yenye upole kuonyesha kwamba mama hakufanikiwa kupata mtoto mzima.

Mifano katika lugha ya Kiswahili;

**43.** **Kiswahili**

*(i)Kuleta kipya*

*(ii)Kujifungua*

*(iii) Kuharibu-kwa maana ya kuavya mimba*

Kuleta kipya inamaanisha kuzaa. Kipya hapa imetumiwa sawasawa na mgeni kwa mfano wa Kikamba hapo juu. Tasfida ya kujifungua pia hutumiwa na katika matumizi yake tumepata kuelewa kwamba, Mama mjamzito huwa amezuilika kutenda na kufanya mambo mengi sana. Hivyo basi matumizi ya tasfida hii huonyesha kwamba, Mama akijifungua huwa na uhuru wa kutenda yale asingeweza kutenda akiwa mjamzito. Kuharibu kumetumiwa kwa maana ya kuavya mimba, hii inadhihirisha upole katika kueleza mwanamke aliyeavya mimba. Tasfida hizi hueleweka tu moja kwa moja kwani ni za desturi na zenye upole mwingi.

Kinyume na tasfida hizi za kueleweka waziwazi kunazo zingine ambazo kwazo msikilizaji huhitaji kuelewa muktadha ili azing'amue. Tasfida hizi kama tulivyogudua katika utafiti wetu zinazua dhana mbili au hata tatu tofauti. Mtumizi wa tasfida hizi huzitumia tu kwa kuzilinganisha na muktadha ili ziweze kueleweka. Tasfida za aina hii ni tasfida zisizo za desturi.

Mfano katika lugha ya Kikamba;

**44.** **Kikamba**

*(i)Musikali*

Tafsiri-askari

*(ii)Kuthumua*

Tafsiri-kupumzika

*(iii)kuvoa*

Tafsiri-kupona kwa maana ya kuzaa

*Musikali* ni tasfida inayomaanisha Askari katika lugha ya Kikamba. Tasfida hii inaweza kuzua aina tofauti za askari, askari wa kawaida, askari mlinzi wa usiku. Katika matumizi itafaa mtumizi atofautishe kwa kutumia muktadha ufaao.

Kwa mfano, "*askari wake alilala lango likafunguliwa na wezi wakamwibia tajiri wake*" kwa kutaja lango na tajiri inaeleweka huyu ni mlinzi wa usiku.

*Kuthumua* kwa maana ya kupumzika, kuzaa, kufa na kulala ni tasfida yenye utata kwani itambidi msikilizaji kutambua muktadha ili kuelewa yanayokusudiwa. Mfano, mama aliyekuwa mgonjwa amepumzika. Matumizi katika muktadha huu yaonyesha amekufa.

Mfano kwa lugha ya Kiswahili;

**45.** **Kiswahili**

*(I)Kupumzika*

*(ii)Mtarajiwa*

*(iii)Nina haja*

Tasfida hii ya *kupumzika* ni tata. Inaweza kutumiwa kuashiria kufa, kupumzika kutoka safari ndefu, kulala na kujifungua. Mtumizi lugha atatofautisha tasfida hio vilevile kwa kutumia muktadha ufaao ndipo msikilizaji atofautishe matumizi yake.

Kwa mfano, mama aliyekuwa mja mzito amepumzika. Hii ni wazi kwamba amejifungua. Mfano mwingine ni, Mzee aliyeugua kwa muda mrefu sasa amepumzika, hii itaeleweka kuwa amekufa.

*Mtarajiwa* ni neno la kumaanisha anayesubiriwa kufika pia inaweza kumaanisha mjamzito. Mtu anaposema *ana haja,* huwa anamaanisha anataka kwenda chooni ama kwa upande mwingine ina maana kwamba mtu anamhitaji mwingine wafanye kitendo cha ngono. Matumizi ya tasfida hizi zote katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili lazima msikilizaji autambue muktadha ndiposa aweze kuitambua maana.

### 3.2.5 Matumizi ya Tasfida za Kikazi/Taaluma

Tulitambua kwamba katika jamii za watumizi lugha ya Kikamba na Kiswahili watu hufanya kazi mbalimabli. Kazi hata ingawa si yenye malipo mazuri hasa kazi za sulubu huonekana duni. Kazi za akili nazo huonewa fahari. Ili kuhifadhi uso wa wafanyi kazi wa sulubu na kuwaonyesha kukubalika, tasfida hutumika ili kuzipa kazi hizo hadhi. Kwa mfano katika lugha ya Kikamba:-

**46.** **Kikamba**

*(i)Mwiitu wakwa*

Tafsiri-binti yangu kwa maana ya Yaya

*(ii)Mundu mue*

Tafsiri-mtu mwerevu kwa maana ya Mganga

*(iii)Musikali*

Tafsiri-askari kwa maana ya Mlinzi

*Mwiitu wakwa* ni tasfida yenye maana ya msichana au binti yangu. Tasfida hii hutumiwa kuashiria Yaya. Kwa kutambulishwa na mwajiri wake kama 'binti' huweza kuhifadhi uso wake na kujihisi mwenye maana na aliyekubalika katika familia hiyo. Kazi aitendayo binti kwao ni kazi ya hiari na ya kwao na huwa si kama mtumwa kwao. Yaya hapa imepanuliwa katika matumizi na pia imedhihirisha upole.

*Mundu mue* katika Kikamba humaanisha mtu mwerevu. Hii ni tasfida ambayo hutumiwa kumtambulisha mganga. Mganga anapoitwa mtu mwerevu kazi yake inalinganishwa na busara na hivyo kuhifadhi uso wake. *Musikali* kwa maana ya mlinzi kwa kupewa jina la askari ambao hufanya kazi zenye mishahara mikubwa ni kupewa hadhi na kuhuhifadhi uso wa mfanyi kazi huyo.

Maneno yale yale yapo katika Kiswahili,

**47.** **Kiswahili**

*(i)Msaidizi kwa maana ya Yaya*

*(ii)Daktari kwa maana ya mganga*

*(iii)Askari kwa maana ya mlinzi*

Yaya kuitwa msaidizi na mganga kuitwa daktari naye mlinzi kuitwa askari, huwapa wafanyi kazi hawa wa sulubu hadhi kuu.  Mganga wa miti shamba kuitwa Daktari kama Muuguzi aliye na elimu ya juu sana basi huhifadhi uso wa mfanyikazi huyo, vilevile tasfida kama msaidizi kwa kuashiria Yaya inampa Yaya hadhi ya juu kwa kuwa mtu wa kupewa msaada huwa amelemewa. Askari hutumiwa kuashiria mlinda lango kwa kumlinganisha na askari wa kawaida kunampa hadhi mlinzi na kuhifadhi uso wake.

### 3.2.6 Matumizi ya Tasfida za Majina ya Wanajamii

Kila jamii huwa na tasfida za majina ya wanajamii ambayo huwaita watu aidha kwa sababu ya heshima ama kwa sababu ya tamaduni zao. Katika utafiti wetu tulipata baadhi ya tasfida zitumiwazo kuwatambulisha wanajamii mbalimbali kama;

**48.** **Kikamba**

*(i)Ng'a Mutuku*

Tafsiri-mjukuu wa Mutuku

*(ii)Muthonua*

Tafsiri-Mkwe

*(iii)Muisikya*

Tafsiri-anayesaidia wananwake kujifungua

Matumizi ya tasfida hizi za majina ya jamii hutokana na pale watu fulani hawafai kuitina majina halisi kwani ni mwiko. Mfano wazazi wa bwana harusi hawafai kumwita mkaza mwana wao kwa jina lake halisi, hivyo basi watamwita jina la heshima kama, *Ng'a Mutuku* kwa maana ya mjukuu wa Mutuku. Bwana harusi naye hafai kuwaita wazazi wa mke wake kwa majina yao halisi. Kwa sababu hii atawaita jina la heshima la *athoni* au *muthonua. Muisikya* ni tasfida inayotumiwa kumtambulisha mwanamke anayewasaidia wanawake kuzaa.

**49.** **Kiswahili**

*(i)Mkaza mwana*

*(ii)Mwinyi*

*(iii)babu*

Katika lugha ya Kiswahili tulitambua kwamba majina mengi yanayotumiwa si tasfida. Hata hivyo kuna tasfida kama mkaza mwana ambayo wazazi wa kijana humwita mke wa kijana kwa sababu ni mwiko kumwita kwa jina lake. Wanawake hawaruhusiwi kuwaita waume zao kwa majina yao halisi. Kwa sababu hio tasfida tofauti tofauti huzuka kama, *mwinyi* kwa maana ya kiongozi wa nyumba. *Babu* nayo ni jina la heshima ambalo laweza kutumiwa na watu wa familia moja kumtambua mzee mwenye nyumba kwani hawafai kumwita kwa jina lake halisi. Tasfida nyingi katika kitengo hiki zilikuwa za kawaida kwani tangu zamani jamii hizi mbili zilitasfidi maneno mengi yaliyokuwa mwiko na kuzitumia kama maneno ya kawaida.

### 3.2.7 Matumizi ya aina mbalimbali za Tasfida zilizotokana na Data ya Kutangamana

Katika kutangamana kwetu na jamii hizi tuliweza kusikia tasfida zifuatazo,

**50. Kikamba**

*(i)Kukunzwa*

Tafsiri-kukunjwa kwa maana ya ndoa isiyo halali(kuwekwa)

*(ii)Kulea liu*

Tafsiri-kukataa chakula kwa maana ya kufa

*(iii)Kuvana mbui*

Tafsiri-kumtia mbuzi alama kwa maana ya kutenda kitendo cha ngono.

Tasfida hizi tulizisikia katika miktadha ya nyumbani lakini sehemu tofautitofauti. Tulipotembelea familia moja iliyokuwa ikifanya kazi ya kuvuna mahindi, kina mama waliongea mambo tofauti. Mama mmoja aliulizwa kile kilikuwa kinaendelea kwa mume

wake kwani haonekani nyumbani. Mama yule alijibu kwa uchungu na kusema, *akunzitwe o vaya kwa Mueni* yaani, amekunjwa hapahapa kwa Mueni. Alitumia tasfida hiyo kumaanisha mume wake amepotelea kwa Mueni ama amechukuliwa na Mueni.

Katika kikao cha wazee nyumbani kwa mzee "Mwalimu" kama alivyoitwa na watu wote kwa sababu alikua mwalimu kwa miaka mingi, ndipo tulisikia tasfida ya *kulea liu*. 'Mwalimu'alikuwa akiwaeleza wale wazee jinsi familia yake ilipitia mambo magumu kisha akasema, *Tata atanalea liu* yaani, kabla ya babangu kukataa chakula, kwa maana ya kabla babake ajafa.

Tulipowatembelea kina mama wakichota maji mtoni, tulisikia mmoja akiwaambia wale wengine kwamba ana haraka kwani mume wake amefika na amemweleza anataka kutia mbuzi alama aharakishe. Mama huyu alisema hivi, "*ninikalaatite kivu natia avika na ambia eenda kuvana mbui."* Kumaanisha nina haraka sana kwani nimeacha chifu amefika na amesema anataka kuweka mbuzi alama. Hii ina maana kwamba, mume wa mwanamke huyu alimhitaji nyumbani haraka ili watende kitendo cha ngono.

Mfano katika Kiswahili:-

**51.** **Kiswahili**

*(i)Babu*

*(ii)Kanitwalie*

*(iii)Kanitilie*

Mfano wa kwanza katika lugha ya Kiswahili, tulipotembelea familia moja, Mzee mwenye nyumba tuliskia akiitwa na kila tuliyempata pale 'Babu' hata mke wake. Neno hili Babu ni neno la heshima kwa mzee aliyekula chumvi nyingi. Walimuita vile

kuonyesha heshima wanayompa na kuonyesha yeye ni tajiri wa watu. Hii ni tasfida ya kuhifadhi uso wa Mzee yule kwa kumsifu.

Mfano wa pili tuliousikia katika familia kadha tulizozitembelea ni tasfida ya *kanitwalie* au *nitwalie.* Hii ni tasfida ambayo ilitumika sana kwa Waswahili kwa maaana ya nichukulie.

Sababu za matumizi haya ni kwamba neno nichukulie si neno lenye heshima ni kama kumwamrisha mtu kufanya tendo lile. Neno hili la kutwaa lina upole sana kwani lina maana ya kushika kitu kwa mkono. Mfano wa tatu tuliousikia ni wa matumizi ya tasfida *kutilia.* Walioitumia sana nyumbani kwa familia tuliyoitembelea na kubahatika kutiliwa chakula cha mchana. Neno kutilia ni neno lililobanwa sana kwani ni kuweka kitu tu mara moja aidha kwa kikombe, chupa au juu ya meza. Tasfida  hii haionyeshi kuchoka katika kutenda tendo lile.

Hii ni tasfida yenye upole kuliko kupakua ambako kwaonyesha kuchoka katika ile hali ya kuchotachota kwa kijiko na kuweka kwenye sahani au bakuli.

Mifano tuliyoitoa hapa ni mifano yenye upole mwingi, inasifu, inaonyesha upendo na kumjali mtu mwingine kwa kuhifadhi uso wake.

### 3.3 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia jinsi tasfida hutumika katika muktadha wa nyumbani katika maisha ya kila siku na upanuzi wake. Tumefanya hivi kwa kulinganisha matumizi ya tasfida za nyumbani katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili.

Tumeshughulikia, kitendo cha usemi, matumizi ya tasfida, kanuni za matumizi ya tasfida, tasfida za; mazingira, sehemu za siri za wanaume na wanawake, hedhi, sherehe za harusi

na nyimbo, tasfida za desturi na zisizo za desturi na tasfida za aina mbalimbali zinazotokana na data za kutangamana. Sura hii ni msingi wa sura ya nne ambapo tutachanganua data kwa msingi wa aina tofauti tofauti tulizozishughulikia katika sura ya tatu. Katika sura ijayo tutashughulikia suala la matumizi ya tasfida katika kufanikisha mawasiliano. Tutashughulikia pia jinsi hulka za kijamii kama vile umri, kazi, jinsia na hadhi huathiri matumizi ya tasfida. Hili tutalifanya kwa kuchanganua data tuliyoikusanya kutoka kwa jamii lugha za Kikamba na Kiswahili.

# SURA YA NNE

# MASIALA YA KIJAMII KATIKA MATUMIZI YA TASFIDA

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inahusu jinsi matumizi ya tasfida hufanikisha mawasiliano, kwa kurejelea masiala ya kijamii kama vile umri, kazi, jinsia na hadhi. Tumefanya hivi kwa kuchanganua data.

Tumeangalia data kuhusu tasfida na matumizi yake katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili. Tumeshughulikia tasfida za majina katika jamii, ujauzito, tasfida za kujamiana, tasfida za magonjwa, tasfida za kifo, tasfida za anatomia na tasfida za takamwili.

Data imewasilishwa kwa majedwali. Majedwali haya yanahusu tasfida katika lugha ya Kikamba na Kiswahili. Tumewasilisha jedwali moja kuhusu tasfida za majina katika jamii, moja ya tasfida za ujauzito na moja kwa kila tasfida za kujamiana, sehemu za siri za binadamu, hedhi, magonjwa, kifo, anatomia na takamwili. Tumefanya hivi ili kuweza kulinganisha matumizi ya tasfida za nyumbani kwa lugha ya Kikamba na Kiswahili kwa urahisi.

## 4.1 Athari za Umri, Jinsia Kazi na Hadhi katika Matumizi ya Tasfida

Matumizi ya tasfida za nyumbani katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili huathiriwa kwa kiwango cha juu na hali za kijamii. Hali hizi ni pamoja na umri, kazi, jinsia na hadhi. Tuliupata ushahidi huu tulipowahoji watafitiwa tofautitofauti. Matokeo ya shuhuda hizi ni kama ifuatavyo:-

### 4.1.1 Umri

Tulitambua kwamba watu wa umri mmoja hawaheshimiani kama ilivyo kwa watu wa umri tofauti tofauti. Watu wa umri mmoja wanapozungumza huwa sio lazima watumie tasfida. Watu wa umri mkubwa wanaruhusiwa kuviita vitu kwa majina ya miiko kwani umri unawaruhusu kuzungumza pasipo kuheshimiana wala kuogopana.

Pale ambapo umri ni tofauti, kwa sababu ya heshima ya walio na umri mkubwa, tasfida hutumiwa kwa wingi ili kudumisha upole na heshima.

Utafiti wetu ulitambua kwamba watu wazima wakisema *'hatutasema mambo hayo hapa kuna watoto'* kumaanisha kunayo maneno ambayo wanaweza kusema wao kwa wao lakini pakiwa na watu wa umri mdogo hawawezi kuyatumia.

Watu wa umri mkubwa kwa upande mwingine hufaa kupewa heshima. Kuna mambo ambayo wameruhusiwa na tamaduni zao kusem pasipo kuwajali watu wa umri mdogo. Watu wazima huyasema mambo fulani pasipo kutumia tasfida na kuchukuliwa kuwa sawasawa.

Kwa mfano mtafitiwa mmoja mwanamke alimwambia binti yake maneno haya*; 'umya katumbulu kaa vaa* we' kwa maana ya ondoa, *katumbulu* ama sehemu ya siri ya kike kwa kuidunisha. Maneno hayo kwa muktadha huo yalionekana sawasawa na hata mtoto hakusikia kukosewa adabu. Kwa kuyatumia maneno hayo huwa hata hawaujali uso wa wadogo zao. Maneno hayo hunenwa waziwazi hasa wanapowapa watoto au watu wa umri ulio chini yao mawaidha, maelekezo au hata wasia. Mambo kama haya yameruhusiwa ingawa yanaathiri pakubwa matumizi ya tasfida. Tulitambua kwamba

nadharia ya Upole hapa pia imekiukwa kwani maneno ya upole yanafaa wanajamii wote kwa jumla.

### 4.1.2 Jinsia

Watafitiwa wengi walitueleza kwamba watu wa jinsia moja wanapozungumza huita vitu jinsi vinavyoitwa, hata kutumia tasfida kwao ni nadra sana kwani huona kwamba wao ni wa jinsia sawa. Utafiti wetu ulitambua kwamba watu wa jinsia moja wanapoongea huwa wanaangalia kama kuna jinsia tofauti karibu nao. Kisha wanasema, "wacha tuambiane ukweli kwa sababu sisi ni kitu kimoja na hakuna tofauti kati yangu na wewe." Kama watu ni wa jinsia ya kike watayasema mambo pasipo woga.

Katika utafiti wetu, tulikuwa na ugumu mwingi kuelezwa mambo na wanaume hasa pale mtafiti mkuu akiwa wa kike. Kunayo heshima katika jamii ya Kikamba na ya Kiswahili baina ya jinsia mbili tofauti. Ilhali watu wa jinsia moja huwa ni rahisi kuelezana chochote kile pasipo kuona haya. Kama ni watu wa jinsia ya kiume hata ingawa vijana na wazee. Matumizi ya tasfida hapa yatakuwa nadra kwani jinsia hii imeshuka na kwa kuyamaliza maneno yao makali kwa kutumia mkakati hasi husema mambo waziwazi pasipo kujali tasfida na basi kuathiri matumizi yake.

Mfano, ni kwa watu wa jinsia ya kike katika lugha ya Kikamba tulipomsikia mwanamke mzima akimwambia binti yake maneno haya "*Wionia andu nondo niki*. Haya maneno yana maana, kwa nini waonyesha watu matiti.  Kwa sababu hapakuwa na jinsia tofauti alipoyanena maneno hayakumuumiza bintiye. Tulitambua kwamba maneno haya yangemuumiza sana bintiye kama kungekuwa na jinsia tofauti.

### 4.1.3 Kazi

Katika kutangamana na watu waliofanya kazi pamoja tuliyatambua mambo haya:-

Watu wanaofanya kazi pamoja hasa kama ni wa cheo kimoja walikuwa na mazoea ya kukaa kama ndugu. Watu hawa walitaniana ili kuifanya kazi yao kufanyika pasipo kuchoka. Kwao huwa kawaida kuyasema mambo waziwazi na kuyachukulia kimzaha, kucheka na kuendelea na kutenda kazi. Mazoea yale ya kukutana kazini kila siku yaliwafanya wasiogopane na kuheshimiana hata ingawa walikuwa wa jinsia tofauti. Walitueleza kwamba katika kufanya kazi pamoja wao pia hukosana na kuambiana maneno yasiyo ya upole. Walisema huyachukulia mambo hayo kama ya kawaida na kuendelea na kazi huku wakitaja msemo wa Kikamba usemao *"mathoka me kathungini kamwe mayiemaa ukungulany'a* yaani, mashoka yalio katika mfuko mmoja hayakosi kugusanagusana. Matumizi ya tasfida hapa huathirika pakubwa kwani si rahisi wafanyi kazi hawa kuyatumia. Sababu ya hali hii ni kuwa katika kazi hasa kazi za kitaaluma maneno mengine huhitaji kuitwa jinsi yanavyoitwa ili pasije pakawa na kutoelewana na kutofahamikiana kwa kazi wanayoitenda.

### 4.1.4 Hadhi

Hadhi ni cheo alicho nacho mtu katika kazi anayoifanya. Tulipowahoji watafitiwa wenye vyeo tofauti tulitambua kwamba watu walio katika cheo kimoja wanaheshima ya kiwango cha chini. Hii ni kwa sababu wao ni watu wa kiwango kimoja. Hivyo, mazungumzo yao yalikuwa waziwazi pasipo na kujali upole sana. Walisema kwamba mtu mwenye cheo na aliye na wadogo zake kazini matumizi yake ya tasfida yataathirika kiasi kikubwa hasa pale yule mwenye hadhi anapoamua ana mamlaka ya kusema mambo

waziwazi kwani si lazima kuwaheshimu wadogo zake. Wale walio chini ya mamlaka kila wakati katika mazungumzo yao watatumia tasfida kwani wako chini ya mamlaka na uongozi wowote ulihitaji kuheshimiwa. Katika tamaduni za Kikamba na Kiswahili, walio mamlakani au wenye vyeo wanafaa kuheshimiwa. Kwa Kiswahili wanapewa majina ya heshima. Kama vile:-

**52.** **Kiswahili**

*i). Mkubwa – Mwenye ukuu, aliye mkuu*

*ii). Bwana – mwenye heshima, mwenye hadhi*

*iii). Kiongozi – mtawala, mwenye kutawala*

*iv) .Mjumbe – mwenye ujumbe*

*v). Mtawala – mwenye mamlaka, mwenye kutawala.*

*vi). Mwenye kiti – kiongozi mwenye mamlaka*.

Utafiti wetu ulibaini kuwa kutokana na majina yale yeyote aliye na hadhi anafaa kupewa heshima na kuzungumziwa kwa upole. Vilevile, hapana sheria yoyote inayomfunga mwenye mamlaka kunena mambo wazi wazi.

Utafiti wetu ulibaini kuwa watu walio na cheo katika Kikamba pia wanapewa majina kama:-

**53.** **Kikamba**

*i). Mutongoi – Kiongozi, anayetangulia*

*ii). Munene – mkuu au mwenye mamlaka*

*iii). Musumbi – mwenye utawala au anayetawala*

*iv). Mwene kivila – Mwenye kiti*

Viongozi huogopwa na kuwekwa juu wakati wote. Utafiti waonyesha kuwa Kuwapa walio mamlakani heshima na kuwazungumzia kwa upole hutokana na utamaduni wa jamii hizi mbili kwa kumwogopa Mungu na kumpa heshima.

Hata hivyo, matumizi ya tasfida yameathiriwa sana kwani viongozi wanapoamua kuyasema maneno jinsi yalivyo, wanayasema pasipo kupingwa. Viongozi wengine walitumia matusi kama kawaida tu na kuathiri matumizi ya tasfida. Vilevile walio chini yao nao ni watu wa kiwango kimoja na waliyazungumza mambo jinsi yalivyo katika uhalisia wake.

## 4.2 Jinsi Tasfida hufanikisha mawasiliano

Kutokana na data tuliyokusanya inadhihirika wazi kwamba matumizi ya tasfida za kinyumbani hufanikisha mawasiliano kwani nia kubwa ya kutumia tasfida ni kuhifadhi nyuso za wengine, kuwasiliana kwa njia ya upole na ya heshima.

Kwa kuweza kuhifadhi uso wa msikilizaji au hadhira, kunayafanya mawasiliano yafaulu. Data tuliokusanya ilionyesha kwamba tasfida kwa kiwango kikubwa zaidi zilitumika kwa sababu ya kuheshimu.

Kwa mfano

Jedwali namba 1.

Matumizi ya tasfida za nyumbani katika lugha ya Kikamb

### 4.2.1 Maoni ya watafitiwa kuhusu matumizi ya tasfida katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili.

**Jedwali namba 1**

| | **Kikamba** | | | | | | | | | | **Kiswahili** | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | K | % | KS | % | H | % | KM | % | BM | % | K | % | KS | % | H | % | KM | % | BM | % |
| Kwa nini tasfida zitumike nyumbani katika lugha ya Kikamba na Kiswahili? | 18 | 90% | 2 | 10% | - | - | - | - | - | - | 17 | 85% | 2 | 10% | - | - | 1 | 5% | - | - |

**Mwongozo**

A – Kuheshimu (K)

B – Kuficha siri (KS)

C – Hazitumiki (H)

D – Kuepuka miiko (KM)

E – Hutumika bila mpango (BM)

Wahojiwa 20= Wanaume naWanawake

Kulingana na data hii inadhihirika kwamba asilimia 87.5 waliohojiwa walitumia tasfida kwa sababu ya heshima ilhali ni asilimia 10 tu waliotumia tasfida kwa sababu ya kuficha siri. Asilimia 2.5 nao walitumia tasfida kwa sababu ya kuepuka miiko.

Kulingana na asilimia hizi ambazo ni jumla ya 100 tunaweza kusema kwamba, heshima, kuficha siri na kuepuka miiko yote ni matendo ya kufanikisha mawasiliano. Data hii inaonyesha matumizi ya tasfida ni ya muhimu sana katika jamii lugha hizi mbili na matumizi hayo yanakusudiwa ili kutimiza kuwasiliana kwa upole.

**4.2.2 Maoni ya watafitiwa kuhusu nyakati tofauti tofauti ambazo tasfida hutumika**

**Jedwali 2**

| | Kikamba | | | | | | | | Kiswahili | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | KZ | **%** | KJ | % | KK | % | KC | % | KZ | % | KJ | % | KK | % | KC | % |
| Wakati wa Mikutano na Sherehe | 10 | 50% | 5 | 25% | 4 | 20% | 1 | 5% | 15 | 75% | 2 | 10% | 2 | 10% | 1 | 5% |
| Wakati wa Matanga | 15 | 75% | 3 | 15% | 2 | 10% | - | - | 15 | 75% | 2 | 10% | - | - | 2 | 10% |
| Wakati wa Tohara | 15 | 75% | 5 | 25% | - | - | - | - | 15 | 75% | 4 | 20% | 1 | 5% | - | - |
| Wakati wa Kazi | 5 | 25% | 5 | 25% | 3 | 15% | 7 | 35% | 4 | 20% | 4 | 20% | 4 | 20% | 8 | 40% |

**Mwongozo**

**A – Kiasi cha juu zaidi (KZ)**

**B – Kiasi cha juu (KJ)**

**C – Kiasi cha kadri (KK)**

**D – Kiasi cha chini (KC)**

**Idadi ya wahojiwa – 20 (umri 18 – 70/ waume kwa wake)**

Data ya jedwali hili yaonyesha kwamba tasfida katika lugha ya Kikamba zilitumika kwa asilimia 56.25 kwa kiasi cha juu zaidi katika shughuli zote zilizoorodheshwa katika jedwali. Matumizi ya tasfida katika shughuli zile zile kwa lugha ya Kiswahili na kwa kiwango cha juu zaidi yalikuwa asilimia 63.75. Kiasi cha juu katika lugha ya Kikamba kilikuwa 22.50 na Kiswahili kilikuwa 15.00. Kiasi cha kadri katika luhga ya Kikamba 11.25 na Kiswahili 8.75. Kiwango cha chini nacho kilikuwa, Kikamba 10 nacho Kiswahili 12.50.

### 4.2.3 Maoni ya watafitiwa kuhusu matumizi ya tasfida kama chombo cha kufanikisha na kuathiri mawasiliano

**Jedwali 3**

| | Kikamba | | | | Kiswahili | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | FZ | **%** | AZ | % | FZ | % | AZ | % |
| Je ,tasfida hufanikisha au huathiri mawasiliano | 38 | 95% | 2 | 5% | 40 | 100% | - | - |

**Idadi ya wahojiwa 20 wanaumena nwanawake**

**Mwongozo**

**A – Hufanikisha zaidi (FZ)**

**B – Huathiri zaidi (AZ)**

Data ya jedwali hii yaonyesha kwamba asilimia 97.5 ya waliohojiwa ilionyesha kuwa matumizi ya tasfida hufanikisha mawasiliano zaidi kwa lugha ya Kikamba na ya Kiswahili. Ni asilimia 2.5 pekee waliosema matumizi ya tasfida huathiri mawasiliano. Kutokana na matokeo ya data hii tunaweza kusema kwamba matumizi ya tasfida za kinyumbani katika lugha ya Kikamba na Kiswahili hufanikisha mawasiliano katika jamii husika.

**4.3 Tasfida za Majina ya jamii kwa lugha ya Kikamba na Kiswahili.**

**Jedwali namba 3**

| | Kikamba | Tafsiri | Kiswahili | Maana |
|---|---|---|---|---|
| Wanaume | *Kivu* | Chifu/kiongozi/mume | Mwinyi<br>(kiongozi),mume | |
| Wanawake | *Ng'a Mutuku*<br><br>*Ng'a Muuo* | Mjukuu wa<br>Mutuku<br>Mjukuu wa muuo | Mkaza mwana<br>Nina | |
| Watoto | *Muthinzio*<br>*Mueni* | Zawadi<br>Mgeni | Zawadi<br>Kipya | |

Tasfida zinazotumika nyumbani hasa kutajia majina ya wanaume, wanawake na watoto huwa hasa zinatumika katika mazungumzo kwa kutomwita mtu kwa jina lake halisi kwani ni mwiko. Matumizi haya huonyesha upole katiaka mazugumzo. Kwa mfano tasfida ya kuita mtu chifu kwa kikamba *'kivu'* inamwonyesha kwamba ndiye kiongozi na anafaa kuheshimiwa kwa nyumba yake. Sawasawa na tasfida inayotumika kwa Kiswahili ni mwinyi ambayo ina maana ya kiongozi.

Watoto nao huwa viumbe tegemezi na pia huonekana kama baraka na ndio sababu hupewa tasfida kama zawadi na mgeni.

### 4.4 Tasfida za Ujauzito.

**Jedwali namba 4.**

| **Kikamba** | **Maana** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| *Kutetheka* | kusaidika | Kujifanya |
| *Kuthumua* | Kupumzika | Kuleta kipya |
| *Kukwata mueni* | Kupata mgeni | Kula amira |
| *Kuvutha* | Kuwa mwepesi | Mtarajiwa |
| *Kuvoa* | Kupona | Kula maharagwe |
| *Kutambaika* | Kuzaa mtoto ambaye hajakomaa na amekufa | Kuavya mimba<br>Kuharibu mimba |

Ujauzito katika jamii hizi hueshimiwa sana ndiposa kukazuka tasfida nyingi kiasi hiki. Ujauzito pia ni matokeo ya tendo la ngono ambalo si la kutajwa hadharani pia. Ni kwa sababu hii basi watumizi lugha wakazua tasfida nyingi ili kuonyesha upole kwa mjazito. Kwa mfano *kukwata Mueni* huashiria kumpokea mgeni ambalo ni jambo la kawaida na wageni hupendwa na watu wengi katika jamii.

**4.5 Tasfida za kujamiana**

**Jedwali namba 5**

| **Kikamba** | **Tafsiri** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| *Kuvitya* | Kukosa/ kutenda kosa | Kwenda safari |
| *Kukoma* | Kulala | Kupanda farasi |
| *Kutonyana* | Kudungana | Kukuna nazi |
| *Kuisana* | Kulana | Kupiga ngoma |
| *Kunewa miio* | Kupewa mizigo | Kuchimbana |
| *Kumanyana* | Kujuana | Kucheza mpira |
| *Kwina na mwenyu* | Kiumba wimbo na mamako | Kupiga maji |
| *Kulisa kitaani* | Kupanda *'kitaa'* | Kufinyana |

Tasfida hizi zimetumika kwa ajili ya kutaja tendo la ngono. Ni tasfida zenye upole mno kwa sababu kwa mfano, *Kukoma* ina maana ya kulala ambalo ni jambo la kawaida kwa kila mtu hivyo wanalitumia kuonyesha upole mwingi. *Kunewa miio* pia humaanisha kupewa mizigo ambako ni kawaida. Mtu akipewa kitu kwake huwa ni faida.

Katika Kiswahili kwenda safari huwa ni jambo la kawaida ambalo atu hupendelea kukuna nazi nako kwaashiria jambo nzuri ambalo laelekea kutengeneza chakula kitamu

kama wali wa nazi. Tendo hili la ngono limezua tasfida nyingi sana kwani ni tendo la aibu na halitendwi hadharani.

Kwa jumla tasfida zote katika kategoria hii zaashiria matendo na hali za kawaida katika jamii yoyote ile na hivyo basi kudhihirisha upole.

## 4.6 Tasfida za Magonjwa

**Jedwali namba 6**

| Kikamba | \|Tafsiri | Kiswahili |
|---|---|---|
| *Thavu* | Dhambi (UKIMWI) | Kuendesha |
| *Kavithe* | Kisonono/kaswende | Pangusa (kaswende) |
| *Ikua* | Kisonono/kaswende | Homa-kisonono |
| *Mwasa mbola* | Mchonga polepole (UKIMWI) | Kutabawali-kujikojolea |
| *Muthelo* | Enye kuisha | |

Kama ilivyo katika kifo katika jamii nyingi ndivyo ilivyo kwa magonjwa kwani ndiyo huaminiwa kuwa chanzo cha kifo au kisababishi cha kifo. Kwa sababu ya woga wa kufa basi magonjwa mengi katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili yametasfidiwa ili kupunguza makali yanayoleta woga.

Kwa mfano: *Kavithe* na *ikua* vyote humaanisha kisonono. Maana ya matumizi haya ni kuficha siri kwa kutumia mafua ambao ni ugonjwa wa kawaida. Kwa upande mwingine katika Kiswahili kuendesha ina upole kwani ni kuashiria kuendesha gari au pikipiki nayo homa ni ugonjwa wa kawaida, hivyo yanatumiwa ili kuashiria upole.

### 4.7 Tasfida za kifo

**Jedwali namba 7**

| Kikamba | Tafsiri | Kiswahili |
|---|---|---|
| *Kwitwa* | Kuitwa | Kutuaga |
| *Kukoma* | Kulala | Kutuacha |
| *Kuthumua* | Kupumzika | Kulala |
| *Kututia* | Kutuacha | Kupumzika |
| *Kutambaasya* | Kunyoosha miguu | Mungu amemuitaji |
| *Kulea liu* | Kukataa chakula | |

Katika jamii nyingi kifo huogopewa na huwa ni mwiko kutumiwa. Hii ndio sababu tasfida nyingi huundwa ili kupunguza makali na kuonyeshwa kama jambo la kawaida. Tasfida nyingi za kifo huacha watu na matumaini kwamba ameenda na huenda akarudi kutoka safarini. Amepumzika, ameitwa na Mungu na ameenda kwenye mjengo. Hii ina maana kwamba makali hupunguzwa na kuwapa watu tumaini kwamba afapo mtu bado

atarudi baadaye. Imani za Wakamba na Waswahili ni kwamba mtu anapokufa anaweza kuzaliwa tena katika jamii na ndiposa jamii hizi huwapa watoto majina ya watu waliokufa ambao wengi wao huwa na tabia zinazofanana na waliokufa.

### 4.8 Tasfida za Anatomia na Sehemu za siri za binadamu.

**Jedwali namba 8**

| | Kikamba | Tafsiri | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| Sehemu za uke | *Miio*<br><br>*Kindu*<br><br>*mbaki* | Mizigo<br><br>Kitu<br><br>tumbako | Kisima<br><br>Kitumbua<br><br>Kitrabu |
| Sehemu za uume | *Muti*<br><br>*Muthi*<br><br>*itumo* | Kijiti<br><br>Mchi<br><br>mkuki | Fimbo<br><br>Msumeno<br><br>Machine |
| matiti | *Kwimba kithui*<br><br>*kuthongooa* | Kifura kifua<br><br>kuchanua | Maziwa<br><br>Kuota tunda |

Sio kila sehemu ya mwili wa binadamu hutasifidiwa. Sehemu zile zinazohusiana na kutumika katika tendo la ngono ndizo huangaliwa kwa aibu na maudhiko. Kwa sababu ya maudhiko hayo viungo hivyo huibua tasfida.

## 4.9 Tasfida za takamwili

**Jedwali namba 9**

| Kikamba | Tafsiri | Kiswahili |
|---|---|---|
| *Makonyoo* | Mkojo | Mkojo |
| *Kyoo* | Choo | Choo |
| *Kiwu* | Maji (mkojo) | Kinyesi |
| *Matuku make* | Siku zake | Hedhi |
| *Kwona mwei* | Kuona mwezi | Hedhi |
| *Aeni* | Wageni | Kuingia mwenzini |
| *Mathina* | Shida | Mvua |

Allan na Burridge (1991) wanasema kwamba mwili wa binadamu hutoa taka ambayo huwa aibu kuzungumuzia. Kuna takamwili tatu kuu. Takamwili hizi ni mkojo, kinyesi na hedhi kwa wanawake. Tasfida ambazo huundwa kutokana na taka mwili huwa ni za upole na zenye kurahisisha mawasiliano. Tasfida nyingi huwa za kawaida na watu wanapozisikia huzielewa moja kwa moja.Utafiti wetu unakubaliana na Allan na Burridge kwani katika matumizi ya tasfida za takamwili tulipata tasfida nyingi na kufahamishwa kwamba ni mwiko kuzitaja takamwili hizo hadharani.

## 4.10 Uchanganuzi wa data

**Jedwali la 10 laonyesha data ya matumizi ya tasfida za kinyumbani katika lugha ya Kikamba. Mikakati ya upole iliyotumika imeonyeshwa pia.**

### 4.10.1 Uchanganuzi wa Data kutokana na Wanaume.

**Jedwali la 10**

| | **KZ** | **%** | **KJ** | **%** | **KK** | **%** | **KC** | **%** | **UC** | **UH** | **UF** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tasifida za majina ya wanajamii | 10 | 50% | 8 | 40% | 1 | 5% | 1 | 5% | √ | | |
| Tasfida za ujauzito | 15 | 75% | 3 | 15% | 1 | 5% | 1 | 5% | √ | √ | |
| Tasfida za kujamiana | 18 | 90% | 1 | 5% | 1 | 5% | - | - | √ | | |
| Tasfida za magojwa | 16 | 80% | 2 | 10% | 1 | 5% | 1 | 5% | √ | √ | |
| Tasfida za kifo | 17 | 85% | 2 | 10% | 1 | 5% | - | - | √ | | |
| Tasfida za anatomia | 18 | 90% | 2 | 10% | - | - | - | - | √ | √ | |
| Tasfida za takamwili | 18 | 90% | 2 | 10% | - | - | - | - | √ | | |

**Mwongozo**

Kiasi ha juu zaidi- KZ

Kiasi cha juu  - KJ

Kiasi cha kadri -KK

**Kiasi cha chini - KC**

**Mikakati**

**Upole chanya - UC**

**Upole hasi - UH**

**Upole fiche - UF**

**Alama √ (mikakati iliyotumiwa)**

**Watafitiwa 20 – wanaume (Lugha ya Kikamba)**

**Jedwali 11 laonyesha data ya matumizi ya tasfida za kinyumbani katika lugha ya Kiswahili. Mikakati ya upole iliyotumika imeonyeshwa pia**

### 4.10.2 Uchanganuzi wa Data kutoka kwa wanaume(Lugha ya Kikamba)

**Jedwali 11**

| | KZ | % | KJ | % | KK | % | KC | % | UC | UH | UF |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tasfida za majina ya wanajamii | 9 | 45% | 10 | 50% | 1 | 5% | - | - | √ | | |
| Tasfida za ujauzito | 16 | 80% | 2 | 10% | 1 | 5% | 1 | 5% | √ | | |
| Tasfida za kujamiana | 20 | 100% | - | - | - | - | - | - | √ | | |
| Tasfida za magonjwa | 15 | 75% | 2 | 10% | 1 | 5% | 2 | 10% | √ | √ | |
| Tasfida za kifo | 18 | 90% | 2 | 10% | - | - | - | - | √ | | |
| Tasfida za anatomia | 18 | 90% | 2 | 10% | - | - | - | - | √ | √ | |
| Tasfida za takamwili | 17 | 85% | 1 | 5% | 2 | 10% | - | - | √ | | |

**Mwongozo**

Kiasi cha juu zaidi- KZ

Kiasi cha juu - KJ

Kiasi cha kadri -KK

Kiasi cha chini- KC

Mikakati

Upole chanya- UC

Upole hasi - UH

Upole fiche- UF

Alama √ (mikakati iliyotumiwa)

watafitiwa 20 – wanaume ( lugha ya Kiswahili)

Kutokana na data ya jedwali hizi mbili, imedhihirika kwamba tasfida za kujamiana, za anatomia na za takamwili ndizo zilizotumika kwa kiwango cha juu zaidi. Asilimia 90.84% ya wanaume walisema tasfida hutumika kwa kiwango cha juu zaidi hasa zinazohusiana na sehemu za siri za mwili wa binadamu, za takamwili kuu tatu na za kitendo cha kujamiana. Kifo kilizua matumizi ya tasfida za kiwango cha juu cha asilimia 85.25 kwani ni janga linaloogopesha katika kila jamii. Hii ni kwa sababu janga hili linamuathiri mwana jamii moja kwa moja na kumtenganisha na maisha.

Tasfida za majina ya wanajamii hazikutumiwa sana kwani ni wanajamii wachache tu waliokuwa na majina ya mwiko. Asilimia 48 ndiyo iliotumia tasfidana hiki ni kiasi cha

kadri. Ujauzito na magonjwa zilizua tasfida za kiasi cha chini kwani kutaja ujauzito na magonjwa mengine hakuupunjui uso wa msikilizaji zaidi.

Asilimia za tasfida za ujauzito zilidhihirika kwa kiwango cha chini cha 5 na kiwango cha chini cha tasfida za magonjwa ni 7.5. Mikakati chanya na hasi hutumiwa kwa tasfida za ujauzito, magonjwa na anatomia. Utafiti huu uligundua kwamba mkakati hasi hutumika pale wanapotumia maneno ya ujauzito kwa mfano,

*'Samahani dada, ulisikia bintiye Abdallah kaavya mimba?'* Kwa kutumia samahani ingawa maneno yatakayofuata si mazuri yatahifadhi uso wa msikilizaji. Katika magonjwa kunayo magonjwa ambayo hutajwa tu kwa majina yake na yasiwe na makali kama mengine. Kwa mfano *"Vijana wengi wanamalizwa na ukimwi.'* Ukimwi ni ugonjwa sugu lakini ukitajwa pasipo kuukamilisha unaonyesha upole hasi. Magonjwa ni hali za kawaida katika jamii na mengine yakitajwa hayana makali mno.

Watu wazima waliruhusiwa kuwaelekeza na kuwapa watoto wao wasia, wanapofanya hivyo wanaweza kutumia maneno ya mwiko na kuzipuuza tasfida. Wanafanya hivyo kwa kuwasiliana pasipo kuupunjua uso wa watoto. Katika mawasiliano hayo upole hasi hutumiwa.

Data hii inaonyesha matumizi ya mikakati katika data tuliyoikusanya

i) Uso chanya – 57.14%

ii) Uso hasi – 42.86%

Hivi ndivyo wanaume wanavyosema. Kwa jumla mikakati ya upole chanya na hasi hutumika kwa asilimia 100. Kuonyesha kwamba tasfida hutumika kama njia ya upole ya kufanikisha mawasiliano.

4.10.3 Data ya matumizi ya Tasfida za nyumbani katika lugha ya Kikamba. Mikakati ya upole iliyotumika imeonyeshwa pia

**Jedwali 12** **Uchanganuzi wa Data kutoka kwa Wanawake**

| | **KZ** | **%** | **KJ** | **%** | **KK** | **%** | **KC** | **%** | **UC** | **UH** | **UF** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tasfida za majina ya wanajamii | 14 | 70% | 2 | 10% | 2 | 10% | 2 | 10% | √ | | |
| Tasfida za ujauzito | 16 | 80% | 3 | 15% | 1 | 5% | - | - | √ | √ | |
| Tasfida za kujamiana | 20 | 100 % | - | - | - | - | - | - | √ | | |
| Tasfida za magonjwa | 15 | 75% | 2 | 10% | 2 | 10% | 1 | 5% | √ | √ | |
| Tasfida za kifo | 18 | 90% | 2 | 10% | - | - | - | - | √ | | |
| Tasida za anatomia | 19 | 95% | 1 | 5% | - | - | - | - | √ | √ | |
| Tasfida za takamwili | 18 | 90% | 2 | 10% | - | - | - | - | √ | | |

Mwongozo

Kiasi ha juu zaidi- KZ

Kiasi cha juu- KJ

Kiasi cha kadri-KK

Kiasi cha chini- K

Mikakati

Upole chanya -UC

Upole hasi- UH

Upole fiche -UF

Alama √ (mikakati iliyotumiwa)

Watafitiwa 20 – Wanawake ( lugha ya Kikamba)

**4.10.4 Data ya matumizi ya Tasfida za nyumbani katika lugha ya Kiswahili.**

**Jedwali la 13**

**Uchanganuzi wa Data kutoka kwa wanawake**

| | KZ | % | KJ | % | KK | % | KC | % | UC | UH | UF |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tasfida za majina ya wanajamii | 14 | 70% | 3 | 15% | 2 | 10% | 1 | 5% | √ | | |
| Tasfida za ujauzito | 15 | 75% | 4 | 20% | 1 | 5% | - | - | √ | √ | |
| Tasfida za kujamiana | 19 | 95% | 1 | 5% | - | - | - | - | √ | | |
| Tasfida za magonjwa | 15 | 75% | 3 | 15% | 1 | - | 1 | 5% | √ | √ | |
| Tasfida za kifo | 18 | 90% | 2 | 10% | - | - | - | - | √ | | |
| Tasida za anatomia | 20 | 100% | - | - | - | - | - | - | √ | √ | |
| Tasfida za takamwili | 19 | 95% | 1 | 5% | - | - | - | - | √ | | |

Mwongozo

Kiasi cha juu zaidi - KZ

Kiasi cha juu - KJ

Kiasi cha kadri -KK

Kiasi cha chini -KC

Mikakati

Upole chanya -UC

Upole hasi - UH

Upole fiche -UF

Alama √ (mikakati iliyotumiwa)

watafitiwa 20 – Wanawake ( Lugha ya Kiswahili)

Uchunguzi wa data inayotokana na wanawake kuhusu matumizi ya tasfida za nyumbani ulidhihirika kupitia jedwali la 12 na 13 kwa kuonyesha kwamba, tasfida za kujamiana, za takamwili na za anatomia zilitumika kwa kiasi cha juu zaidi. Asilimia yake ilidhihirisha ukweli huo. Asilimia 95 kwa lugha ya Kikamba na Kiswahili 95. Kwa jumla asilimia 95 kwa lugha hizo mbili.

Wanawake waliohojiwa walisema tasfida zilitumika kwa kiwango cha juu zaidi. Tasfida za kifo zilifuata kwa asilimia 90 kwa lugha ya Kikamba na asilimia 90 kwa lugha ya Kiswahili. Jumla ya asilimia 90 walitumia tasfida za kifo.Tasfida za ujauzito zilidhihirika kwa asilimia 85.25 kwani wanawake waliona haya kuyataja mambo yanayowahusu hasa mbele ya jinsia tofauti au umri tofauti.

Tasfida za magonjwa na majina ya jamii zilikuwa katika kiwango cha chini cha asilimia 70.25.

Mikakati ya upole vilevile ilitumika ambapo,

i) Uso chanya ulitumika kwa asilimia 57.14

ii) Uso hasi nao ulitumika kwa asilimia 42.86

iii) Kwa jumla mikakati ya upole chanya na hasi ilitumika kwa asilimia 100

**4.10.5 laonyesha Data ya matumizi ya tasfida za nyumbani katika lugha ya Kikamba.**

**Jedwali 14 Uchanganuzi wa Data kutoka kwa Vijana (watoto)**

| | KZ | % | KJ | % | KK | % | KC | % | MIKAKATI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | UC | UH | UF |
| Tasfida za majina ya wanajamii | 15 | 75% | 2 | 10% | 1 | 5% | 2 | 10% | ✓ | | |
| Tasfida za ujazito | 15 | 75% | 3 | 15% | 2 | 10% | _ | _ | ✓ | ✓ | |
| Tasfida za kujamiana | 18 | 90% | 2 | 10% | _ | _ | _ | _ | ✓ | | |
| Tasfida za magonjwa | 15 | 75% | 2 | 10% | 1 | 5% | 2 | 10% | ✓ | ✓ | |
| Tasfida za kifo | 15 | 75% | 2 | 10% | 2 | 10% | 1 | 5% | ✓ | | |
| Tasfida za anatomia | 18 | 90% | 1 | 5% | 1 | 5% | _ | _ | ✓ | ✓ | |
| Tasfida za takamwili | 18 | 90% | 2 | 10% | _ | _ | _ | _ | ✓ | | |

**<u>Mwongozo</u>**

**Kiasi cha zaidi - KZ**

**Kiasi cha juu -KJ**

**Kiasi cha kadiri -KK**

**Kiasi cha chini -KC**

**Mikakati**

**Upole chanya -UC**

**Upole hasi - UH**

**Upole fiche -UF**

**Watafitiwa 20- wanarika (Lugha ya Kikamba)**

**4.10.6 Data ya matumizi ya Tasfida za kinyumbani katika lugha ya Kiswahili. Mikakati ya Upole iliyotumika inaonyeshwa pia.**

**Jedwali 15 Uchanganuzi wa Data kutoka kwa Vijana Wanarika (watoto)**

| | | | | | | | | | MIKAKATI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | KZ | % | KJ | % | KK | % | KC | % | UC | UH | UF |
| Tasfida za majina ya wanajamii | 16 | 80% | 4 | 20% | – | – | – | – | ✓ | | |
| Tasfida za ujauzito | 17 | 85% | 1 | 5% | 1 | 5% | 1 | 5% | ✓ | ✓ | |
| Tasfida za kujamiana | 18 | 90% | 1 | 5% | 1 | 5% | – | – | ✓ | | |
| Tasfida za magonjwa | 14 | 70% | 2 | 10% | 2 | 10% | 2 | 10% | ✓ | ✓ | |
| Tasfida_za kifo | 17 | 85% | 2 | 10% | – | – | 1 | 5% | ✓ | | |
| Tasfida za anatomia | 18 | 90% | 2 | 10% | – | – | – | – | ✓ | ✓ | |
| Tasfida za takamwili | 17 | 85% | 1 | 5% | – | – | 2 | 10% | ✓ | | |

**Mwongozo**

**Kiasi cha juu zaidi - KZ**

**Kiasi cha juu - KJ**

**Kiasi cha kadiri - KK**

**Kiasi cha chini - KC**

**Mikakati**

**Upole chanya - UC**

**Upole halisi - UH**

**Upole fiche - UF**

**Watafitiwa 20 wanarika (Lugha ya Kiswahili)**

Matokeo ya data ya wanarika katika lugha ya Kikamba na Kiswahili

Wanarika wengi walipata tasfida zikitumiwa na hawakuwa na uhakika kwa nini zilitumika. Kwao, waliziona kama lugha ya kawaida. Hata ingawa waliziona tasfida kama lugha ya kawaida, uchunguzi huu ulibainisha kwamba tasfida za kujamiana, za anatomia na za takamwili zilitumika kwa kiasi cha juu zaidi. Wanarika waliyakopa maneno mengine kutoka lugha ya Sheng' na hata ya Kiingereza kuelezea maneno hayo waliyoyaona ya aibu kwao. Utafiti huu haukueleza kwa nini waliyaona maneno hayo yakiwa ya aibu.Ilibainika kwamba hata katikati ya hao wanarika walitumia tasfida hizi za mkopo.

**Mfano wa tasfida za mkopo kwa vijana:**

| 54. | **Kikamba** | **Tafsiri** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| | -*kukuna muvila* | -kucheza mpira | -kwa maana ya kitendo cha ngono |
| | -*kuthauka kalata* | -kucheza karata | -kwa maana ya kitendo cha ngono |
| | -*kukuna ngoma* | -kucheza ngoma | - kwa maana ya kitendo cha ngono |
| | -*Ena muvila* | - ana mpira | -ana mpira kwa maana ya ana mimba |

**55. Kiswahili**

-*Kunyesha*- hedhi

-*kucheza gemu*- kutenda kitendo cha ngono

-*kucheza boli*- kutenda kitendo cha ngono

-*kufinyana*- kutenda kitendo cha ngono

Hata hivyo wanarika walizitumia tasfida hasa za kujamiana, anatomia na za takamwili kwa asilimia 90 kwa lugha ya Kikamba na kwa lugha ya Kiswahili asilimia 88.3 jumla ni asilimia 89.15.

Tasfida za majina ya wanajamii kwa lugha ya Kikamba zilitumika kwa asilimia 75 na asilimia 80 kwa lugha ya Kiswahili. Hata ingawa kwa lugha ya Kikamba ni mwiko kuwataja wazazi kwa majina yao halisi, utafiti huu ulibainisha kwamba watoto wakati fulani fulani waliwaita wazazi wao kwa majina yao halisi au hata kuwaita kwa majina ya baba zao kwa utani.

Kwa mfano:

| 56. Kikamba | Tafsiri |
|---|---|
| -*Mwiitu wa Mutisya* | - Bintiye Mutisya |
| -*Mwanaa Mueni* | - Mwana wa Mueni |
| -*Muendi* | - Jina- Muendi |
| -*Muvoye* | - Jina- Muvoye |

Kwa upande mwingine, utafiti huu uligundua kwamba vijana Waswahili waliwaheshimu wazazi wao zaidi na hawakuweza kuwaita kwa majina yao. Waliwaita majina ya heshima kama:-

**57. Kiswahili**

-*Nina - Mama*

-*Abu - Baba*

-*Wavyele-Wazazi*

Matumizi ya tasfida za ujauzito kwa Kikamba yalikuwa asilimia 75 na asilimia 85 kwa Kiswahili. Magonjwa na kifo vile vile yalizua matumizi ya tasfida kwa sababu yaliogopwa sana na wanajamii. Tasfida za magonjwa ni asilimia 70.25 kwa watumizi wa Kikamba na Kiswahili ilhali ya kifo ni asilimia 80 kwa watumizi wa Kikamba na Kiswahili.

Mikakati ya upole ilidhihirika kutumika kwa asilimia 100.

Mfano:

i. Mkakati chanya - 57.14%

ii. Mkakati hasi- 42.86%

Vijana walidhihirisha kwamba tasfida ni njia ya kuwasiliana kwa upole. Hii inadhihirisha hata pale wanapojaribu kuunda tasfida za mkopo ili waweze kuwasiliana kwa njia ya upole.

**4.11 Muhtasari wa matokeo ya Data**

Tunaweza kubaini mikakati miwili ambayo imetumika katika uchanganuzi wa data yetu. Mikakati hii ni

a) Mkakati wa uso chanya

b) Mkakati wa uso hasi

Mikakati hii ilitumika kwa aslimia 100 kwa jumla. Mikakati hii ndiyo inayodhihirisha nadharia ya Upole kama wanavyosema Penelope na Levinson (1978).

Nadharia ya upole ni nadharia inayojali uso wa wengine na kuhakikisha kwamba mawasiliano yametendeka kwa upole na kuyafanikisha. Haya yamedhihirika katika matumizi ya tasfida za kinyumbani katika lugha za Kikamba na Kiswahili.

Tasfida kwa jumla hutumiwa ili kuepuka kutaja na kutumia maneno yenye aibu na mwiko katika jamii. Kwa kufanikisha mawasiliano, kila mtumizi lugha hutumia tasfida. Hii ni njia ya kuonyesha kuwajali wengine, kuwaheshimu na kuwatambua.

Data tuliyoikusanya na kuchanganua imeonyesha kuwa katika watumizi lugha ya Kikamba na Kiswahili, tasfida hutumiwa kwa kiasi cha juu zaidi. Asilimia 90 na zaidi. Asilimia 100 katika kutumia tasfida hutumia mikakati ya upole. Hii ni thibitisho kwamba kila jamii hutumia lugha kama jamii nyingine na huwajali wanajamii, kwa hivyo

huhakikisha matumizi ya tasfida yamezingatiwa. Mtu asiyetumia tasfida katika jamii huonekana kama mwenye kichaa na asiyefaa katika jamii hiyo.

### 4.12 Hitimisho

Katika sura hii ya nne tumeonyesha jinsi matumizi ya tasfida hufanikisha mawasiliano, jinsi hali za kijamii kama umri, jinsia, kazi na hadhi huathiri matumizi ya tasfida na tumechanganua data tofautitofauti kuhusu aina za tasfida kama zinavyotumika katika muktadha wa nyumbani. Kwa kufanya hayo tumeweza kupata matokeo kwamba tasfida za lugha ya Kikamba na ya Kiswahili hutumika kwa jinsi moja na kuna uhusiano mkubwa katika matumizi yake.

Katika sura ifuatayo tunashughulikia muhtasari wa mahitimisho, changamoto na mapendekezo ya tafiti za baadaye.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI WA MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Kwa kutumia data, tumeonyesha jinsi kulivyo na uhusiano mkubwa katika matumizi ya tasfida tofautitofauti za muktadha wa nyumbani. Tumeonyesha jinsi hali za kijamii zikiwemo umri, jinsia, kazi na hadhi zaweza kuathiri matumizi ya tasfida na pia tumechanganua na kuonyesha jinsi tasfida tofauti hutumiwa na wanajamii kwa misingi ya nadharia ya Penelope na Levinson ya Upole.

Vilevile tumeonyesha jinsi mikakati ya Upole chanya na Upole hasi hufikiwa katika matumizi ili kuhifadhi uso wa msikilizaji na hadhira kwa jumla.

Katika sura hii tunatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti, changamoto za utafiti, mapendekezo na kutamatisha utafiti huu uliokuwa unalinganisha matumizi ya tasfida za kinyumbani katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili kwa kurejelea nadharia ya Upole ya Penelope na Levinson (1978).

## 5.1 Muhtasari wa Matokeo

Utafiti huu ulikuwa unalinganisha matumizi ya tasfida za muktadha wa nyumbani katika lugha ya Kikamba na Kiswahili. Katika utafiti wetu tulikuwa na lengo la kuchunguza jinsi matumizi ya tasfida za nyumbani hufanikisha mawasiliano na iwapo hali  za kijamii kama umri, jinsia, kazi na hadhi huathiri matumizi ya tasfida.Tulikuwa na lengo la kujibu maswali matatu makuu:-

- Je, kunao uhusiano mkubwa katika tasfida zitumiwazo katika muktadha wa kinyumbani katika lugha ya Kikamba na Kiswahili?

- Je, matumizi ya tasfida zitumiwazo katika muktadha wa kinyumbani huweza kufanikisha mawasiliano?

- Je, hali za kijamii za umri, jinsia, kazi na hadhi huathiri matumizi ya tasfida katika muktadha wa nyumbani?

Kutokana na matokeo ya data, inadhihirika kwamba watumizi lugha hizi mbili za Kikamba na Kiswahili hutumia tasfida kwa sababu ya kumheshimu Mola na kuheshimiana wao kwa wao kwa hivyo, msingi wa kuunda tasfida na kuzitumia katika jamii hizi mbili ni heshima. Haya yamedhihirishwa na matokeo ya data ambayo ni asilimia 87.5 ya kutumia upole katika mawasiliano.

Ilibainika kwamba tasfida nyingi zimeundwa kutokana na vitu na vifaa vilivyo katika mazingira ya jamii lugha za Kikamba na Kiswahili. Matumizi ya tasfida za aina tofauti tofauti kama vile za sehemu za siri za mwili wa binadamu, hedhi, kifo, anatomia na takamwili yalikuwa na uhusiano mkubwa. Hii ni kwa sababu watumizi lugha walidhihirisha kwa asilimia 100 kutumia tasfida kwa upole kwa kiwango cha juu zaidi.

Jamii hizi mbili pia zilidhihirisha kutumia tasfida zilizofanana kwa kuashiria kitu kimoja. Kwa mfano, katika kueleza hedhi kwa wanawake walitumia *kuona mwezi*, katika kifo walitumia tasfida kama*, kulala, kupumzika na katika* ujauzito walitumia tasfida kama;

*-Kujifungua*

*-kupata mgeni sawa na kupata kipya*

*-kupumzika*

Uchunguzi huu unaonyesha kwamba tendo la kujamiana lilizua tasfida asilimia 100 kwa jamii lugha ya Kikamba na asilimia 90 kwa jamii lugha ya Kiswahili jumla ya asilimia 95 kuliko aina zingine. Hii ni kwa sababu tendo hili lilionekana la aibu kuliko vitendo vingine katika jamii.

Tasfida kwa jumla zilitumiwa ili kuhifadhi uso wa msikilizaji na kufanikisha mawasiliano pasipo kuupunjua uso wa msikilizaji na tena kwa njia ya upole. Uchunguzi wetu vilevile ulionyesha hali za kijamii kama umri, kazi, jinsia na hadhi huathiri matumizi ya tasfida kwani katika umri mmoja, wafanya kazi wa cheo kimoja na pia jinsia moja hujiona watu wa kiwango kimoja na huweza kupuuza kutumia tasfida kwani heshima kati yao ni ya kiwango cha chini mno.

Hadhi nayo huweza kuathiri matumizi ya tasfida pakubwa kwa sababu ya kutumia cheo vibaya. Uchunguzi huu pia uligundua kwamba matumizi ya tasfida za nyumbani huwa ni kwa ajili ya kupunguza makali na kuhifadhi uso wa mwengine kama wanavyosema Penlope na Levinson (1978). Haya yamedhihirishwa na data ya mikakati ya upole chanya na upole hasi ambayo ilitumika kwa kiasi cha juu zaidi, cha jumla ya asilimia 100. Hii ina maana kwamba, watu wakizungumza katika jamii lugha mbili hizi huwa wanafuata sheria zisizoandikwa lakini zipo katika tamaduni zao. Hii inaonyesha umahiri walio nao watumizi lugha na ubunifu wa kutumia lugha pasipo na sheria.

## 5.2 Changamoto za Utafiti

Utafiti huu ulikubwa na chagamoto chungu nzima, hata hivyo mtafiti alijifunga kibwebwe tena na tena na kuhakikisha ameukamilisha. Changamoto kuu ilikuwa

tamaduni za Waswahili ambazo haziwaruhusu wanaume kutangamana na mwanamke asiye wa aila yao na kudadisiwa au kuhojiwa. Jambo hili lilimpa mtafiti chagamoto kwa sababu alikuwa wa kike. Kila alipomhoji mwanamme alimwelekeza kwa mke au bintiye ili kupata maelezo kwao. Mwanamme msaidizi aliyetumiwa kama mtafiti alisaidia ingawa hatuwezi kuwa na uhakika wa yale aliyoyakusanya. Waswahili ni waumini wa dini ya kiislamu na kila mtafiti alipotangamana nao alionekena na kushukiwa kama anayeweza kuwa anadadisi au kuchunguza, mambo fulani ya siri.

Mtafiti alitambulika kwa mavazi aliyovaa. Mtafiti huyu alipojaribu kuvalia buibui alitambulika na kuambiwa ni kumkirihi Mtume, yaani ni chukizo kwa Mola.

Swala la tasfida ni swala ambalo haliwezi kushughulikiwa pasipo kutaja mwiko. Wengi walionekana kuwa na shaka kwa nini mtu atake kujua mananeo yanayotokana na mwiko, na hasa yanayohusu sehemu za siri za binadamu, kifo, hedhi, magonjwa na anatomia. Jambo hili lilizua shaka na watafitiwa wengi waliona haya kujibu maswali na kufikia hata kuziacha nafasi katika hojaji. Jambo hili lilivunja moyo sana lakini mtafiti alijitahidi hadi tamati na kukusanya data ya kutosha.

Muda wa kukusanya data ulikuwa changamoto pia kwani sehemu hizi mbili ziko mbalimbali na muda ulikuwa mfupi mno. Kwa sababu hii utafiti huu haungeweza kukusanya data kwa watafitiwa wengi kama vile tungependa.

### 5.3 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya data tuliyokusanya tumetambua kwamba, matumizi ya tasfida ni muhimu sana katika kila jamii, kila jamii inatia juhudi za kuimarisha na kuyaendeleza maadili. Hivyo basi twapendekeza tasfida za lugha ya Kikamba na ya Kiswahili ziundiwe

kamusi kwani maneno mengi yanaendelea kufa na kuathiriwa na lugha ya Sheng’ na ya kiingereza. Twapendekeza pia waandishi wa vitabu vya shule za msingi na za sekondari waongeze mada za tasfida katika vitabu vinavyotumiwa mashuleni na katika vyuo. Kuongeza mada kutawapa wanafunzi wengi msingi wa matumizi bora ya tasfida.

Matumizi ya tasfida hulenga kurahisisha mawasiliano, kuwasiliana kwa njia mwafaka, kuhifadhi uso wa msikilizaji na kuwasiliana kwa upole. Ni kwa sababu hii tunapendekeza zaidi kila sera inayotagusana na binadamu kutilia mkazo mafunzo ya tasfida. Sera kama za elimu, za matibabu, makanisa na mashirika ya kibinafsi, kuzingatia mafunzo ya tasfida kutapunguza vifo, vita na chuki vinayoletwa na kutofautiana kwa mazungumzo na lugha isiyo na upole.

Utafiti wetu ulijikita katika kulinganisha matumizi ya tasfida za lugha mbili tu, Kikamba na Kiswahili. Utafiti huu pia ulijibana kwa muktadha wa nyumbani pekee. Utafiti zaidi unaweza kufanywa katika miktadha mbalimbali inayohusu shughuli zingine za binadamu kama vile, matibabu, shuleni, vituo vya magari, sokoni na michezoni. Utafiti mwingine unaweza kuhusu ulinganishi wa matumizi ya tasfida, maana za tasfida katika jamii tofauti za kibantu na za Kiswahili. Utafiti wetu unapendekeza utafiti zaidi katika kulinganisha matumizi ya tasfida katika vituo vya redio vya Kikamba kama Musyi FM na vya Kiswahili.

**MAREJELEO**


Allan K. and Burridge.K. (1991) *Euphemism and Dysphemism.*New York: Oxford University Press.

Brown, Penelope & Stephen Levinson (1978) *Politeness! Some Universal in Language Usage.* Cambridge University Press

Chiraghdin S. na Mnyampala M. (1977*). Historia ya Kiswahili.* Oxford University Press. Nairobi.

Gatambuki, M.G.(2010) *A cognitive linguistic Analysis of Gikuyu euphemisms*. M.A Kenyatta University. Unpublished.

Guthire, M (1948*). Classification of Bantu Languages*. London International Africa Institute Press.

Halliday. M.A.K (1978) Language as a Sociosemiotic. *The social Interpretation of Language and Meaning*. London Edward Arnold and Stoughton.

Harry, H. (1954) *Language in Culture.* Chicago: The University of Chicago Press.

Hudson (1995) *Language and Society* London: Macmillan Publishers.

Hymes, D (1964*) A Language, Culture and Society*: New York: Harper and Row Publishers.

Khatibu S. Mohamed (1983). *Historia ya Maendeleo ya Kiswahili Zanzibar*. Lugha ya Kiswahili toleo Dar es Salaam.

Kothari, C (2004) *Research Methodology* ($2^{nd}$ rev. edition) *New Age Technology* Press

Leech, Geoffrey (1983) *Principles of Pragmatics:* London: Longman.

Mesthrie, R (Ed) (2002). *Coincise Encyclopedia of Sociolinguistics*. Amsterdam.

Mutiga, J. (2002) *The Tone System of Kikamba Phonology*, A case Study of Mwingi Dialect. Unpublished PhD Thesis University of Nairobi

Mugenda, O (2003) *Research Methods, Quantitative Aproaches*: Acts Press Nairobi

Mutiso, K (2005) *The Nature of Forbidden Language*, A paper presented at the Symbosium Organized by the University of Nairobi.

Mwangi, P. (2003) *A description of Non Cooperatives In Legal English in Kenya based on Grice's principle of Cooperation*. Unpublished M.A Thesis, University of Nairobi.

Njeri, S. (2007) *A Pragmatic Analysis of Gikuyu Lexical Euphemisms in HIV/AIDS Discourse* Unpublished M.A Thesis, University of Nairobi.

Stock Well, P (2008) *Sociolinguistics.* A Resource Book for Students London Routledge.

Trudgill P (2000) *Sociolinguistics*: *An Introduction to Language and Society* 4th ed. London: Penguin books.

TUKI (2006) *English Swahili Dictionary* (3rd edition) Der.es.salaam: TUKI.

TUKI. (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Usami, M (2000 6d) *Discourse Politeness Theory and Cross Cultural Pragmatics.*

Wambua, R.S (2009*) Variation in Dialectical use of and Attitudes toward Taboo Words and Euphemism in Kikamba.* Unplished M.A project U.O.N.

Wardhaugh, R (2002) *An Introduction to Sociolinguistics*. (4th Ed). Oxford: Blackwell Publishers.

Whitely, W (1969) *Swahili the Rise of a National Language*, Mthuen and Co. Ltd.

_________ (1974) *Language in Kenya Nairobi:* Oxford University Press.